

2009

MADA: MTINDO KATIKA NYIMBO ZA KAZI

ZA JAMII YA WARABAI

MWASILISHI: MURIUKI NAOMI KUVUNA

**PENDEKEZO LA UTAFITI LILILOANDIKWA KWA MADHUMUNI
YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA
UZAMILI YA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

APRIL 2013

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu na haijawahi kuwasilishwa kwa minajili ya kupata shahada katika chuo kikuu chochote.

JINA: MURIUKI NAOMI KUVUNA

NAMBARI: C50/CE/11257/07

SAHIHI

.....

TAREHE


3rd / 5 / 2013.....

WASIMAMIZI

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi waliochaguliwa na chuo

JINA: PROF. G.K. KING'EI- IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA
KIAFRIKA, CHUO KIKUU CHA KENYATTA

SAHIHI:

.....

TAREHE:

3/5/2013.....

JINA: PROF. C.M. NDUNGO- IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA
ZA KIAFRIKA, CHUO KIKUU CHA KENYATTA

SAHIHI:

.....

TAREHE:

3/5/2013.....

TABARUKU

Naitabaruku tasnifu hii kwa mpendwa mume wangu Evanson Muriuki kwa mapenzi yasiyo kifani pamoja na watoto wangu niwapendao Derrick Muriithi, Daisy Njeri na David Munene kwa kunihimiza na kunipa moyo wa kuendelea na elimu yangu.

SHUKRANI

Kwanza kabisa ningependa kutoa shukani zangu kwa Rabuka kwa kunipa uhai, neema na moyo wa kujiendeleza katika masomo haya. Utukufu na sifa ni kwake daima.

Pili natoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu Prof. King'ei na Prof. Ndungo kwa kuniongoza vyema na mashauri murua nilipokuwa nikitayarisha kazi hii. Pia ningependa kumshukuru Dkt. Ryanga kwa kunihimiza na kunipa moyo kuendelea na kazi hii. Sitamwacha mhadhiri Ngesu kwa ushauri wake nilipokuwa naendelea na masomo haya. Mungu wa rehema awabariki sana.

Vile vile natoa shukrani maridhawa kwa mpenzi mume wangu bwana Evanson Muriuki aliyenisaidia kwa hali na mali. Shukrani kwa kunionyesha upendo na kunitia moyo kukamilisha masomo yangu. Sitawasahau wanangu Derrick, Daisy na David kwa uvumilivu wao nilipokuwa chuoni na pia kunipa mazingira yenye afya ya kielimu.

Shukrani zingine ziwaendee wazee wa vijiji nilikofanyia utafiti hasa mzee Chengo na Ndaro. Pia dada Ruth, Sarah, wifii Mechizi na Mrs. Nguma na wazazi walinitia moyo pamoja na ndugu zangu na shemeji wote.

Shukrani za mwisho ziwaendee wanafunzi wenzangu. Shukrani za kipekee ziwaendee Rachel Maina, Fredrick Mayore, Prisca Chebet, Gladys Kinara, Beth, Muchiri na Ng'etich kwa kunisaidia kwa kila hali kufanikisha kazi yangu.

Mwisho kabisa nampa mkono Bi. Mary Khaemba na Violet Aloo kwa uvumilivu wao wa kunipigia chapa kazi hii. Mungu awabariki sana.

UFAFANUZI WA ISTILAHU

- Hodiya** : Nyimbo zinazoimbwa na watu wanapofanya kazi mbalimbali kama vile kulima, kuvuna, kutwanga, kusaga n.k.
- Wawe** : Nyimbo zinazoimbwa wakati wa kilimo.
- Kimai** : Nyimbo zinazohusishwa na shughuli za baharini.
- Honda** : Kuponda nafaka.
- Tanzu/Utanzu** : Vipengele mbalimbali zinazoshughulikiwa katika kazi za fasihi simulizi
- Kipera** : Vipengele mbali mbali vinavyoshughulikiwa katika kila utanzu wa fasihi simulizi.
- Mtindo** : Jumla ya ubunifu unaojitokeza katika kazi yoyote ya fasihi.
- Kaya** : Makazi walimoishi jamii ya Wamijikenda na pia ni sehemu maalum za maabudu.

IKISIRI

Nyimbo ni kipera muhimu cha ushairi katika fasihi simulizi. Nyimbo hutofautiana kulingana na maudhui, lugha na wahusika. Sifa moja ambayo hubainisha nyimbo ni matumizi yake ya lugha ya tamathali kama vile methali, taashira, tashbihi, sitiara na jazanda miongoni mwa nyingine.

Ingawa tafiti mbalimbali za nyimbo zimefanywa kama vile: nyimbo za arusi, bembelezi, nyiso au nyimbo za tohara, mbolezi, katika jamii mbalimbali, hata hivyo kwa ufahamu wetu, hodiya au nyimbo za kazi hazijafanyiwa utafiti wa kina na hasa kwa upande wa kuchunguza mbinu za kimtindo katika jamii ya Warabai. Katika tasnifu hii tumechunguza mbinu za kimtindo katika nyimbo za kazi za jamii ya Warabai.

Katika sura ya kwanza, tumetoa usuli wa mada, swala la utafiti, sababu za kuchagua mada, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia miongoni mwa mambo muhimu ya kikaida.

Katika sura ya pili tumeangazia chimbuko na utamaduni wa jamii ya Warabai. Umuhimu wa kutoa maelezo haya ni kuwa mambo ya nyimbo za kazi huambatana na utamaduni wa jamii yoyote ile. Tumeeleza shughuli mbalimbali za kikazi katika jamii hii.

Katika sura ya tatu tumeangalia tafsiri ya nyimbo mbalimbali za kazi pamoja na kuangalia matumizi ya lugha na mbinu za kimtindo zilizotumika. Tumeshughulikia

nyimbo kumi na tano kama data ya kuonyesha jinsi nyimbo hutumika katika kazi za jamii ya Warabai.

Tumetamatisha tasnifu kwa sura ya nne ambapo tumetoa muhtasari wa kazi hii, matokeo ya utafiti na mapendekezo. Vivyo hivyo tumeeleza changamoto tulizokumbana nazo katika utafiti huu.

YALIYOMO

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0	Usuli wa mada.....	1
1.1	Swala la utafiti.....	2
1.2	Maswali ya utafiti.....	3
1.3	Malengo ya utafiti.....	3
1.4	Sababu za kuchagua mada.....	3
1.5	Upeo na mipaka ya utafiti.....	4
1.6	Misingi ya nadharia.....	4
1.7	Yaliyoandikwa kuhusu mada.....	6
1.8	Mbinu za utafiti	12
1.8.1	Maktabani.....	12
1.8.2	Utafiti wa nyanjani.....	13
1.8.3	Uteuzi wa sampuli.....	13
1.8.4	Ukusanyaji wa data.....	14
1.8.5	Uchanganuzi wa data.....	14
1.8.6	Uwasilishaji wa data.....	15

SURA YA PILI: JAMII YA WARABAI

2.0	Utangulizi.....	16
2.1	Makazi ya Warabai.....	17
2.2	Maisha ya ndoa na mavazi.....	19
2.3	Nyimbo na ngoma.....	19
2.4	Kazi na shughuli za wanajamii.....	20
	• Ujenzi wa nyumba.....	20
	• Kulima, kutwanga na kusaga.....	21
	• Utengenezaji wa makuti.....	22
	• Ufugaji.....	22
	• Usasi.....	23
	• Uchumaji.....	25
	• Uwekaji wa nyuki na uvunaji wa asali.....	26
	• Ufumaji wa vikapu na mikeka.....	27
	• Uvuaji wa samaki.....	27
	• Hitimisho.....	27
	Tanbihi.....	28

SURA YA TATU

UCHANGANUZI WA MBINU ZA KIMTINDO KATIKA NYIMBO ZA KAZI ZA JAMII YA WARABAI

3.0	Utangulizi.....	29
3.1	Uchanganuzi wa nyimbo za kazi	31
3.2	Juhudi katika kazi.....	31
3.3	Ufugaji	39
3.4	Ugemaji.....	47
3.5	Ujenzi wa nyumba.....	50
3.6	Mawaidha ya kazi.....	52
	Hitimisho	58

SURA YA NNE

HITIMISHO

4.0	Utangulizi.....	60
4.1	Muhtasari wa utafiti.....	60
4.2	Matokeo ya utafiti.....	61

4.3	Mapendekezo.....	64
4.4	Changamoto za Utafiti huu.....	65
	Hitimisho.....	66
	Marejeleo.....	68
	Kiambatisho 1.....	77
	Kiambatisho 2.....	78
	Kiambatisho 3.....	79
	Kiambatisho 4.....	105

SURA YA KWANZA

1.0 Usuli wa mada

Nyimbo ni kipera katika utanzu wa ushairi. Mojawapo ya malengo ya elimu ni kutambua, kudadisi, kudhamini na kustawisha aina za tanzu mbalimbali za lugha na fasihi kwa jumla. Kwa hivyo utafiti wa nyimbo za kazi katika jamii ya Warabai, utakidhi lengo hili.

Kwa mujibu wa Wamitila (2008) nyimbo zina historia ndefu katika jamii zetu. Anasema nyimbo zilianza tu mara binadamu alipopata lugha na kuweza kuzieleza na kuzifumbata hisia zake.

Kipera cha nyimbo kimefasiriwa kwa njia mbalimbali. King'ei na Kisovi (2005), wanaeleza wimbo kama utungo ambao una mpangilio maalum wa maneno na una mahadhi. Huweza kuimbwa na mtu mmoja au kikundi. Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004) inasema nyimbo ni maneno yanayotamkwa kwa sauti za muziki.

Nyimbo huwa ni za aina mbalimbali kama vile: Bembelezi, mbolezi, nyiso, nyimbo za harusi, za kisiasa, za mapenzi, za watoto na za kazi. Msokile (1993), akizungumzia nyimbo za kazi anasema tabia hii ya kuimba wakati wa kazi ilishamiri sana wakati wa ujima.

Nyimbo huwa na maudhui mbalimbali na huendelezwa kwa mbinu za kimitindo tofauti tofauti. Wamitila (2008) anasema maudhui ni jumla ya masuala au mambo yanayoshughulikiwa katika kazi za fasihi. Masuala haya hutokana na jinsi mtunzi au

mwandishi anavyoikuza mada ambayo ni misingi wa kazi yake kupitia matumizi ya lugha mbalimbali.

Katika kazi hii tumeshughulikia zaidi kigezo cha mbinu za kimtindo katika nyimbo za kazi za jamii ya Warabai. 'Mtindo' kwa mujibu wa Wamitila (2003) ni njia anayotumia mwandishi kuwasilisha ujumbe wake. Uchunguzi wa mtindo unaweza kuhusisha tashbihi, takriri, balagha, jazanda, istiari, uundaji wa sentensi na kadhalika.

1.1 Swala la utafiti

Jamii za Kiafrika huwa na nyimbo za kitamaduni ambazo hudhihirisha majukumu mbalimbali.

Finnegan (1970) anathibitisha wazo hili kwa kusema kuwa shughuli nyingi za binadamu kama vile: harusi, tohara, mazishi, kulima na kuvuna hushirikisha nyimbo. Miongoni mwa majukumu ya nyimbo ni kuhimiza wafanyao kazi kujitahidi na kuendelea kufanya kazi bila ulegevu na pia kuleta umoja.

Tafiti ambazo zimefanywa za Kimijikenda, zimejikita zaidi katika isimu na sio fasihi kwa mfano, Ngowa (2007) ameshughulikia vitenzi vya Kigiriyama. Watafiti wengine wengi wameshughulikia aina tofauti za nyimbo kama za harusi, Mbogo (2008), 'Nyimbo za harusi za Waembu'. Simiyu (2007) ametafiti nyimbo za tohara. 'Nyiso za Wabukusu'.

Hata hivyo kwa ufahamu wetu, nyimbo za kazi hazijafanyiwa utafiti wa kina hususan katika jamii ya Warabai. Kwa hivyo kuna umuhimu wa kufanya utafiti wa kina kuhusu nyimbo za kazi katika jamii ya Warabai, hasa kwa kuzingatia mbinu za kimtindo.

1.2 Maswali ya utafiti

Utafiti huu ulilenga maswali yafuatayo:

- Ni shughuli zipi za kikazi zilizoandamana na nyimbo?
- Watunzi wa nyimbo za kazi za jamii ya Warabai walitumia mbinu gani za lugha?
- Ni mbinu gani za kimtindo zilizotumika katika utunzi wa nyimbo za kazi za jamii ya Warabai?

1.3 Malengo ya utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo yafuatayo:

- Kueleza baadhi ya shughuli za kikazi zilizoandamana na nyimbo.
- Kuratibu matumizi ya lugha katika nyimbo za kazi za jamii ya Warabai.
- Kuratibu mbinu za kimtindo katika nyimbo za kazi za jamii ya Warabai.

1.4 Sababu za kuchagua mada

Kulingana na ripoti ya Bakari (1988), kuhusu fasihi simulizi ya Mijikenda, inasema;

“Wamijikenda kama kabila lolote la Kenya, wana utamaduni mkuu wa fasihi simulizi. Fasihi hii haijawekwa kwa maandishi. Urithi wa fasihi hii ya Mijikenda uko katika hatari ya kuangamia kama hatua mwafaka hazitachukuliwa kuihifadhi na kuikuza.”

(Tafsiri yetu)

Kwa vile nyimbo za kazi hazijashughulikiwa vilivyo kama za harusi, tohara, bembelezi, tuliona ni vyema kuzishughulikia kwa kugemea zaidi kuchunguza mbinu za kimtindo. Umuhimu wa utafiti huu wa nyimbo za kazi ni kuzihifadhi katika fasihi

simulizi. Utafiti pia utasaidia kuongeza ufahamu wa fasihi simulizi kwa wanafunzi wa shule za upili, vyo vikiu na wapenzi wa fasihi simulizi kwa ujumla.

1.5 Upeo na mipaka ya utafiti

Utafiti kuhusu mbinu za kimtindo za hodiya ulijifunga katika vijiji vitano ambavyo ni makazi ya Warabai. Utafiti wenyewe ulifanyiwa sehemu za Kokotoni, Somali, Mazeras, Kisurutini na Ruruma (Kombeni). Hii ni kwa sababu baada ya Wabantu kutoka Shungwaya na Kuja mwambao wa Pwani, Warabai walianza kuishi sehemu tulizoshughulikia.

Mtafiti ameshughulikia makundi mbalimbali kama vile wanaume, wanawake na vijana wakati wa kazi zao tofauti tofauti. Nyimbo walizozimba wakati wa kazi hizi, ndizo zilizotafitiwa mbinu mbalimbali za kimtindo.

1.6 Misingi ya Nadharia

Kwa mujibu wa King'ei na Kisovi (2005), kuna mwingiliano mkubwa kati ya tanzu nne za fasihi simulizi, yaani hadithi, semi, maigizo na ushairi. Kimtindo na kimuundo zote hutumia maneno ya lugha kwa njia ya kimaumbo na kitamathali. Nadharia ni dira ya mtafiti inayomwongoza katika utafiti wake ili apate jawabu kwa swala linalotafitiwa.

Utafiti huu umetumia nadharia ya kimtindo. Nadharia hii hushughulika na matumizi ya lugha

kwa maana ya nje na pia kwa maana ya ndani. Kuna waasisi kadha wa kadha ambao wameeleza nadharia hii. Coombes (1953) anasema, lengo la mtindo ni uchunguzi wa lugha na kanuni zake ili kubainisha mbinu zilizotengwa kwa kazi fulani ya jamii kueleza sababu za kipengee fulani kutumiwa na vingine kutotumiwa. Anaongeza kusema mhakiki lazima azingatie vipengee vinavyofanya kazi iwe na mnato. Kupitia maelezo haya ya Coombes, tulipata kuwa nadharia hii ilitufaa kuchanganua matumizi ya lugha na mbinu za kintindo katika nyimbo za kazi za jamii ya Warabai.

Mwendelezi mwingine wa nadharia hii ya kintindo ni Leech (1969). Yeye anakiri kuwa fasihi haiwezi kuchanganuliwa bila kutizama matumizi ya lugha. Kazi ya fasihi hukusudia kuwasilisha hisi au tajriba fulani kwa wasomaji au wasikilizaji. Maelezo haya pia yalitufaa katika utafiti wetu wa matumizi ya lugha na mbinu za kintindo katika nyimbo za kazi za jamii ya Warabai.

Muasisi mwingine wa kintindo ni Ngara (1981). Anaeleza kuwa nadharia hii hujihusisha na mambo ya kiisimu na pia ya kifasihi. Ameeleza mtindo kuwa ni namna ya kujieleza kwa kutumia lugha, yaani jinsi mwandishi (mwimbaji) awasilishavyo ujumbe wake. Kwa mujibu wa Ngara, nadharia hii ina vipengele au mihimili kadha wa kadha. Mihimili yenyewe kama inavyoelezwa na Ngara ni:

- Kiwango cha kifonolojia ambacho hushughulikia uchambuzi wa mfumo wa sauti katika lugha.

- Kiwango cha msamiati ambapo mtafiti hujishughulisha na uteuzi wa mbinu kama vile jazanda, taswira, methali, semi, tashbihi, istiari na maana zake.
- Kiwango cha urasmi wa msemi.
- Kiwango cha sarufi ambapo huchunguza aina za sentensi na uhusiano kati ya maana na muundo.
- Kiwango cha maandishi ambapo mambo kama vile chapa, rangi, alama zinazochapishwa, uakifishaji na aya hushughulikiwa ili kumvutia msomaji wa kazi ya sanaa.

Katika utafiti huu tuliongozwa na mihimili miwili ile ya msamiati na sarufi. Tuliamua kutumia viwango hivyo viwili kwani vingetuongoza katika utafiti wetu, yaani kuchunguza matumizi ya lugha na mbinu za kimtindo. Wanamtindo husisitiza mtindo wa lugha kama chombo tekelezi kinachosaidia katika kuelewa ujumbe uliokusudiwa. Lugha huchangia ufanisi wa kazi ya sanaa kwani hutumiwa katika uzuaji wa ubunifu wa kifasihi.

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Baadhi ya waandishi na watafiti wameshughulikia kazi za fasihi simulizi hasa nyimbo katika jamii mbalimbali za Kiafrika. Hata hivyo fasihi simulizi inahitaji utafiti zaidi kama wanavyosema Nandwa na Bukenya (1983):

"Utanzu wa fasihi simulizi haswa wa Kiafrika haujafanyiwa utafiti mwingi ukilinganishwa na fasihi andishi."

Wanjiku Kabira na Karega Mutahi (1988), wameandika kuhusu fasihi simulizi ya Wakikuyu katika kitabu, 'Gikuyu Oral Literature'. Katika kitabu hiki walizingatia nyimbo za vijana wa kiume na wa kike, kuhusu mungu waliemwamini. Nyimbo zingine zilihusu wakoloni na mateso waloyoyapata kutokana na wakoloni walionyakua ardhi yao. Waliandika pia nyimbo za kuwasifu watu mashuhuri kama Kenyatta na Waiyaki waliopigania ardhi yao (uk. 152-3). Hawakushughulikia nyimbo za kazi za jamii hii.

Naye Chesaina (1999), ameandika fasihi simuzi ya Wakalenjin. Amezungumzia bembelezi (uk. 108). Pia ametafiti nyimbo za tohara (nyiso) za jamii hii. Ameandika kuhusu nyimbo za harusi-nyimbo hizi ziliimbwa na wageni waalikwa katika harusi. Amedondoa nyimbo za istiara ambazo zinasuta walevi wanaotukanana wanapolewa au kutokuwa na uaminifu katika ndoa. Ametafiti nyimbo za kisiasa na nyimbo za kidini katika jamii hii. Hata naye hakushughulikia nyimbo za kazi katika jamii hii.

Naomi Kipury (1983), ameandika fasihi simulizi ya Wamaasai. Katika maandishi yake anasema:

“Nyimbo na ushairi ni sehemu muhimu sana ya maisha ya jamii nyingi. Katika jamii ambozo zimejikita katika utamaduni wao, kuna ada ambazo hutekelezwa zikiandamana na nyimbo na mashairi” (uk. 190)

Naomi ameshughulikia nyimbo zifuatazo: Bembelezi, nyimbo za kukashifu vijana waliokataa kupashwa tohara, nyimbo za akina mama za maombi. Ana nyimbo za

kuwasifu mashujaa na za mapenzi.Kwa hivyo Naomi hakushughulikia hodiya katika jamii hii.

Waandishi wengine wa hivi karibuni pia wamezungumzia kipera cha nyimbo.King'ei na Kisovi(2005),wameshughulikia nyimbo za kimapokezi(za kitamaduni).Nyimbo hizi hupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na huwa ni mali ya jamii nzima.Wameshughulikia mifano ya nyimbo za harusi,mapenzi,nyiso,nyimbo za kidini au sala kwa Mungu,nyimbo za maombolezi,bembelezi,mawaidha,za kukashifu maovu ya jamii miongoni mwa nyingine.Pia wameshughulikia aina mbalimbali ya nyimbo za kisasa.

Vile vile watafiti kadhaa wametafiti uwanja huu wa nyimbo.King'ei (1992) ametafiti: Muundo, majukumu na matini katika nyimbo za Taarabu nchini Kenya; miaka ya 1963-1990. Utafiti huu ulitufaa kwa kuzingatia lugha inavyotumika katika nyimbo. Ulitofautiana na wetu kwani hatukujadili kuhusu maudhui ya nyimbo hizo.

Kinoti (2008), ameandika kuhusu nyimbo za harusi, tohara, bembelezi na nyimbo za kidini miongoni mwa nyingine. Ametaja tu mifano ya kazi mbalimbali katika jamii ya Wameru na Wamaasai bila kutoa mifano ya nyimbo zenyewe. Hata hivyo katika kutizama mifano hiyo ya kazi alijikita zaidi katika maudhui yake na wala sio mbinu za kintindo kama ilivyo katika kazi yetu.

Wamitila (2008) ameandika nyimbo kama vile bembelezi, za mapenzi, nyiso na pia nyimbo za kazi kwa kifupi. Amekuza zaidi wazo la maudhui kuliko matumizi ya lugha na mbinu za kimtindo.

Watafiti kadhaa wameshughulikia kipera cha nyimbo kwa mada zifuatazo: Nkonge (1988), alitafiti fani na maudhui katika nyimbo za Joseph Kamaru. Utafiti wake ulitufaa hasa kwa upande wa fani. Hata hivyo utafiti wake ni tofauti kwani huyu ni mwimbaji wa kibinafsi na nyimbo tulizoshughulikia ni za jamii.

Ntarangwi (1990), ameshughulikia nyimbo za kisiasa. Alijijhusisha na maudhui katika nyimbo za Ramadhan 'Mtoro' Ongara. Alibainisha jinsi kazi ya fasihi simulizi inavyoyapa maudhui uzito kuliko fani. Utafiti huu ulitofautiana na wetu kwani hatukujikita katika maudhui bali matumizi ya lugha na mbinu za kimtindo, hata kama tafiti ni za nyimbo.

Uchunguzi wa maudhui ya nyimbo za John Mwale ulifanywa na Yalwala (1991). Kazi yake ilijikita katika maudhui ya kijamii. Aliangalia maudhui mbalimbali katika nyimbo za Mwala. Utafiti huu pia ulitofautiana na wetu kwani tulishughulikia zaidi mbinu za kimtindo katika nyimbo za kazi.

Kadhalika Wambua (2001), ametafiti Mtindo wa nyimbo za Kakai Kilonzo. Utafiti huu ulitufaa kutambua mitindo mbalimbali ya nyimbo. Utafiti wetu haukuangalia mtindo kwa upana kama alivyofanya Wambua. Ulitofautiana na wetu kwani nyimbo zetu ni za kijamii. Ameangalia mtindo kama mtu mwenyewe, baina ya kauli kadha, kama ukiushi wa kaida na mitindo kama njia ya kujieleza.

Mutwiri (2005), ametafiti mitazamo ya utendakazi wa nyiso katika jamii wa Watigania. Utafiti wake ni tofauti na wetu kwani alishughulikia majukumu au maudhui ya nyimbo hizo za nyiso na wala si matumizi ya lugha na mbinu za kimtindo.

Mtafiti mwingine ni Simiyu (2007). Ametafiti kuhusu nyiso za Wabukusu; maudhui na lugha. Anaeleza nyimbo kutegemea jinsi wakati unavyobadili maudhui na lugha. Utafiti wake ulitufaa kwa upande wa matumizi ya lugha lakini ulikuwa tofauti kwani kazi yetu haikujikita kwa maudhui wala kuangalia mabadiliko ya lugha kiwakati.

Mwanzia (2007) ametafiti Mtindo wa nyimbo za watoto wa shule za chekechea. Katika kuangalia mtindo ameshughulikia maudhui, sentensi, msamiati na tamathali za semi. Utafiti ulitufaa kuelewa mitindo katika nyimbo. Utafiti wake ulitofautiana na wetu kwani zetu zilikuwa ni nyimbo za kazi kwa watu wazima na vijana.

Malenya (2008) ametafiti matumizi ya lugha na jazanda katika nyimbo za Jacob Luseno. Ameonyesha kwamba lugha na jazanda anazotumia zinaafikiana na matukio katika vipindi vyote vya utawala nchini Kenya. Utafiti huu ulitufaa hasa kwa kuzingatia lugha inavyotumika katika nyimbo.

Kobia (2008), ameshughulikia taswira za Kiuana za wanaume miongoni mwa Waigembe. Pia ametafiti taswira za mwanamke na mwanamume katika nyimbo za tohara za wanaume katika nyimbo za Waigembe. Utafiti huu ulitofautiana na wetu kwani haukushughulikia lugha na mbinu za kimtindo za nyimbo hizo.

Nyimbo za harusi zimeshughulikiwa na Mbogo (2008). Ametafiti Mabadiliko ya maudhui kiwakati katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu. Utafiti wake pia ulitofautiana na wetu kwani haukushughulikia matumizi ya lugha na mtindo katika nyimbo hizo.

Wathome (2008) ametafiti mtindo katika nyimbo za tohara za jamii ya Wakamba wa Masaku tarafa ya kati. Utafiti huu ulitufaa kwani mtindo ndio tuliojadili katika utafiti wetu, tofauti ni kuwa zetu ni nyimbo za kazi.

Mwingine aliyetafiti nyimbo ni Rajwayi (2009). Ameshughulikia maudhui na mtindo katika Nyimbo za Faustin Munishi. Utafiti ulitufaa kwa upande wa lugha. Utafiti huu ulitofautiana na wetu kwani hatukujadili maudhui kwa undani katika nyimbo za kazi.

Mutegi (2010) ametafiti Maigizo katika fasihi simulizi mfano wa *kirarire* katika nyimbo za tohara za Wameru. Utafiti wake japo ni nyimbo, ulitofautiana na wetu kwani hakuzingatia mambo ya lugha na mbinu za kimtindo.

Mwisho tuna Mwaniki (2011) ambaye ametafiti matumizi ya lugha katika nyimbo tohozi za Salim Junior. Utafiti wake ulitufaa kwa upande wa lugha, japo ulitofautiana kwani nyimbo tulizoshughulikia zilikuwa za kienyeji na sio za kutoholewa.

Kutokana na tafiti hizo zote za nyimbo, hakuna utafiti ambao umefanywa kuhusu nyimbo za kazi, kama asemavyo Finnegan (1970) kuwa; "Kuna haja ya utafiti wa nyimbo za kazi katika jamii ya Waafrika" uk. 206-207.

1.8 Mbinu za utafiti

Sehemu hii ina maelezo kuhusu data ilivyopatikana, hatua za kuikusanya data, uchanganuzi wa data na jinsi data ilivyotafsiriwa ili kutimiza malengo ya utafiti.

Utafiti ulihusisha mbinu kuu mbili za uchunguzi. Ule wa maktabani na pia nyanjani.

1.8.1 Maktabani

Utafiti wa maktabani umejumuisha kutembelea maktaba na makavazi ya kitaifa jijini Nairobi kwa kusudi la kupata maandishi ya kihistoria yanayohusu jamii ya Warabai.

Maandishi juu ya fasihi simulizi kwa jumla kutoka jamii mbalimbali yalipitiwa kwa kina ili kumpa mtafiti mwangaza zaidi juu ya utanzu huu wa ushairi, yaani nyimbo. Vitabu, majarida, tasnifu zozote zilizohusiana na nadharia ya kimtindo zilisomwa. Kazi hizi za maktabani zilitupa mwongozo ambao ulihusiana na utanzu wa nyimbo, nadharia ya kimtindo, mihimili mahsusi ya nadharia na vile tulivyopaswa kuitumia.

1.8.2 Utafiti wa nyanjani

Nyanjani tulikutana na jamii ana kwa ana. Utafiti wa nyanjani ulitusaidia katika kukusanya data, yaani nyimbo za kazi za Warabai, kuchanganua sampuli iliyotumika na hata uwasilishaji wa data hiyo kulingana na swala la utafiti na malengo ya utafiti. Mbinu ya uchunzaji ilitumiwa pamoja na mahojiano yasiyo na muundo.

1.8.3 Uteuzi wa sampuli

Utafiti huu umeelekezwa maeneo matano wanamoishi Warabai. Maeneo haya ni Kokotoni, Somali, Mazeras, Ruruma na Kisurutini. Hizi ni sehemu ambapo Warabai wanaishi baada ya kutoka Shungwaya.

Sampuli yakini ya kimaksudi ilitumiwa. Hapa kilichotuongoza katika uteuzi wa sampuli hii

ni sababu fulani maalum alizonazo yaani kuchunguza matumizi ya lugha na mbinu za kimtindo, Mugenda na Mugenda(2003). Kwa upande wetu, tulichagua makundi mbalimbali yakishiriki katika shughuli tofauti tofauti kama kulima, kutwanga na kusaga.

Tuliteua makundi ya akina mama, wazee, vijana katika kazi zao na kuwaomba waimbe walipokuwa wakifanya kazi hizo. Hawa ni wake na waume wenye umri wa juu. Kwa hivyo pia tulitumia sampuli viwango.

Katika makundi hayo yote tumeshughulikia nyimbo kumi na tano. Idadi hii ilikidhi malengo ya utafiti na wahojiwa waligawanywa kama ifuatavyo: Nyimbo za kulima, kutwanga na kusaga. Nyimbo za ufugaji na ujenzi. Nyimbo za ugemaji na uvunaji asali. Sehemu hiyo na idadi ya makundi ilichaguliwa kwa sababu ilimpa mtafiti data ya kutosha kama asemavyo Milroy (1987), kwamba sampuli ndogo ndiyo mwafaka.

1.8.4 Ukusanyaji wa data

Vifaa kama kaseti ya kurekodi nyimbo ilitumiwa. Kulikuwa pia na kalamu na daftari ya kunakili yale ambayo hayakurekodiwa. Mahojiano yasiyoratibiwa yalitumika hasa kupata historia ya Warabai na shughuli zao. Data ilikusanywa pia kupitia uchunguzi wa kushiriki ambapo mtafiti alishiriki katika shughuli mbalimbali za kazi katika jamii husika.

1.8.5 Uchanganuzi wa data

Uchanganuzi wa data ulitarajia kutimiza malengo ya utafiti na kutoa majibu ya maswali ya utafiti (Brymann na Crammer, 1997).

Mtafiti amechanganua data kwa kuzingatia nyimbo alizorekodi. Alizingatia matumizi ya lugha na mbinu za kimtindo katika nyimbo hizo. Aliichanganua data hiyo kupitia ufafanuzi na maelezo ya moja kwa moja.

1.8.6 Uwasilishaji wa data

Baada ya kuorodhesha nyimbo za kazi zilizoimbwa na Warabai matumizi ya lugha na mbinu za kimtindo zilishughulikiwa. Taarifa iliyohusiana na nyimbo hizo imeelezwa kwa maandishi ya maelezo na ufafanuzi, kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Matokeo ya utafiti huu yameelezwa kikamilifu katika sura ya mwisho ya tasnifu.

SURA YA PILI

2.0 Utangulizi

Sehemu hii ni muhimu ili kuelewa jamii inayofanyiwa utafiti kwa mfano mambo kadhaa yanayohusiana na jamii hii kama vile: Maeneo ya kijiografia, ndoa, mavazi, sherehe zao, dini na muhimu zaidi shughuli mbalimbali za kikazi. Kwa hivyo tumetizama utamaduni wa Warabai kwa lengo la kufahamu swala la utafiti na malengo yake.

Warabai wamepakana na Wachonyi, Wajibana, Wakambe, Waribe na Wakauma kwa upande wa kaskazini. Upande wa kusini wamepekana na Wadigo. Upande wa kaskazini mashariki wamepekana na Wagiriama. Upande wa Magharibi wamepakana na Waduruma. Upande wa mashariki wamepakana na mji mkuu wa Mombasa.

Utamaduni kwa mtazamo wa kijamii ni mfumo wa maisha ya wanadamu wanavyoishi na kutangamana na wanajamii wenza. Ngugi (1987), anasema utamaduni hauhusishi tu hadithi au ngano za watu wa kale bali hujihusisha na mahusiano na shughuli mbalimbali za kijamii.

Katika Kamusi ya Kiswahili sanifu (2010) inaeleza kuwa utamaduni ni mila, asili, jadi na desturi za kundi la jamii fulani. Maelezo haya yanatuonyesha kuwa kwa ujumla utamaduni ni, namna watu walio hai wanavyoendeleza maisha yao katika asasi mbalimbali za jamii kuambatana na mazingira.

2.1 Makazi ya Warabai

Warabai ni kundi moja la Mijikenda. Hawa ni Wabantu wakaaji wa Pwani. Jina Mijikenda ni la Kiswahili linalomaanisha miji tisa au makundi tisa, nayo ni: Giriama, Ribe, Duruma, Rabai, Kambe, Digo, Kauma, Jibana na Chonyi.

Asili ya Warabai (Mijikenda) ikiwa ni pamoja na makabila ya Kibantu wanayopakana nao huhusishwa na baadhi ya wanahistoria na misitu ya Kongo (Were na Wilson 1991). Nadharia ya Kongo inadai kuwa Wamijikenda, Wakikuyu, Wameru, Wapokomo, Wakamba na jamii zingine zilizohusiana zilihama kutoka Kongo na kuingia Kenya kupitia katikati ya ziwa Victoria na milima ya Taita. Baadaye makundi haya yaliamia Pwani ya Kenya na kukusanyika mahali palipoitwa Shungwaya.

Ongezeko la watu lilisababisha jamii hizi kutawanyika sehemu mbalimbali za Kenya. Walitoka Shungwaya upande wa kaskazini na kuelekea kusini, walipoishi katika kaya. Kila kundi lilikuwa na kaya lake lililoingiwa kwa vijia vyembamba. Kila kaya lilikuwa na koo sita. Kaya zilikuwa na mfumo wa serikali zilizoanza kuvunjika karne ya kumi na saba walipoanza kuhama mijini.

Katika miaka ya 1940, jamii zilizowazunguka Wamijikenda waliwaita 'watu wa Nyika', kinyume na Waswahili walioishi mijini. Wamijikenda na Waswahili walichukuliwa kama ni watu wa kundi moja.

Baadhi ya wanahistoria kama Spear (1948), waliamini kwamba Warabai na Waduruma hawakutoka Shungwaya hata ingawa wenyewe walikiri kuwa walitoka huko. Warabai walijulikana zaidi kwa uzoefu wa kugema. Jina 'Rabai' linatokana na kisa kuwa kulikuwepo mama mmoja aliyekuwa akinywa 'mnazi' sana na akasikika akisema, "raha ii siiricha" yaani siwezi kuwacha raha hii ya unywaji. Kutokana na jina 'Raha ii' (1) likaja kubadilika na kuwa Rabai.

Warabai, Wagiriama, Wajibana, Wakambe, Wakauma, Wachonyi na Waribe ni wakaaji wa wilaya ya Kilifi. Waduruma na Wadigo wako wilaya ya Kwale.

Rabai imegawanyika katika vijiji mbalimbali ambavyo huwakilishwa na chifu. Wamegawanyika katika mbari mbili kuu: Mbari ya uume na mbari ya ukwe. Mbari ya Uume ni wale wenye baba wa Kirabai na Mbari ya Ukwe ni wale wenye mama wa Kirabai. Baadhi ya mbari zipatikanazo kwa kundi la Warabai ni: Mbari ya Tsui, Mwajohadzuya, Mkadhiaka, Mwamumba, Mtiga, Mwadaha, Mkavyo, Mvitsa, Mwaruri miongoni mwa nyingine. Kijana alipopitia tohara, ndiyo alikubalika kuwa mmoja wa koo hizo.

Warabai walimwamini Mungu waliyemwita Mulungu. Waliabudu mizimu walioaminika kuathiri sana maisha ya walio hai. Manabii kati ya Warabai waliitwa "wafisi."

Warabai pia walikuwa na vikundi walivyoitwa 'kambi'(2) Wazee hawa walisuluhisha migogoro yoyote katika jamii. Ilikuwa ni kama mahakama kuu. Pia walijishughulisha na mambo ya kidini na sherehe katika jamii. Kambi pia ingetangaza vita kwa jamii yoyote

ambayo ingeonyesha uchokozi. Makundi ya marika yaliunda wapiganaji na kuinga jamii hii kutokana na maadui. Muundo wa koo au mbari ulisaidia kutia nguvu umoja wao.

2.2 Maisha ya ndoa na mavazi

Jamii iligawanyika katika makundi mbalimbali. Kundi la watoto hawangetangamana na vijana au hata wazee katika mikutano yao. Hawakuruhusu watu kuoana kutoka mbari moja. Wazee ndio waliowachagulia vijana mabibi. Hata hivyo ndoa ziliruhusiwa kati ya makundi hayo tisa. Ndoa za wake wengi ziliruhusiwa na waliheshimu sana wakuu wao.

Mavazi ya kitamaduni kwa upande wa akina mama yaliitwa 'Mahando'. Wazee walivaa mashuka waliyoyatandaza kama mtindo wa Kikoi. Ingawa kutokana na maendeleo, wengi wameacha kuvalia mavazi haya.

2.3 Nyimbo na ngoma (3)

Kinoti (2008), anasema katika utamaduni wa Kiafrika, nyimbo zilipamba sherehe na tamasha mbalimbali. Nyimbo hizi ni zao la shughuli za binadamu pamoja na hisia zake na hivyo huzingatia miktadha tofauti tofauti.

Warabai waliamini Mungu waliyemwita Mulungu. Waliabudu mizimu walioaminika kuathiri sana maisha ya wanajamii. Manabii waliopatikana katika jamii hii waliitwa "Wafisi".

Warabai walikuwa na vikundi vya wazee waliyoitwa 'kambi'. Wazee hawa walisuluhisha migogoro yoyote katika jamii. Ilikuwa kama mahakama kuu. Pia walijishughulisha na mambo ya kidini na sherehe katika jamii. Kambi pia ingetangaza vita kwa jamii yoyote ambayo ingeonyesha uchokozi. Makundi ya marika yaliunda wapiganaji na kukinga jamii hii kutokana na maadui. Muundo wa koo au mbari ulisaidia kutia nguvu umoja wao.

Warabai wana utajiri mkuu wa aina mbalimbali za nyimbo na ngoma kama vile: Mabumbumbu, Mchechemeko, Gonda, Sengenya, Mwanzele, Chela, Vunja Mkebe, Tunungu, Dundika, Kiri ngongo, Mudzumbano, Bango, Msego miongoni mwa nyingine.

2.4. Kazi na shughuli za wanajamii

Licha ya nyimbo na ngoma katika sherehe mbalimbali kama za mazishi, harusi, kumpa mtoto jina na tafrija nyingi, uimbaji huweza kufanywa wakati wa kufanya kazi tofauti tofauti.

Ujenzi wa Nyumba:

Nyumba za Warabai zilijengwa kwa udongo uliofinyangwa na kupigiliwa katikati ya miti, iliyosimamishwa kwa ustadi walizoziezeka kwa kutumia makuti- majani yaliyosukwa kutoka kwa minazi. Ujenzi wa nyumba ulifanywa kwa ushirikiano wa vijana. Vijana walikusanyika wakajenga bila malipo. Malipo yao ni chakula tu kutoka kwa anayejengewa nyumba hiyo. Tulishuhudia wakijenga kwa furaha na hata kuimba nyimbo za kujitia moyo kuendelea na kazi hiyo.

Kulima

Awali ardhi ilikuwa imemilikiwa na mbari nzima. Mtu angeweza kufyeka na kulima sehemu ya ardhi ambayo haitumiwi na mwingine. Shughuli muhimu zaidi ilikuwa ni kilimo. Kuchimba, kupanda, kupalilia na kuvuna kulifanywa na wanaume na wanawake. Wanaume walifanya kazi upande wao na wanawake walifanya upande mwingine wa shamba hilo. Shughuli hizi zilihita nguvu na pia zilikuwa kazi za kukera. Ili kuweza shughuli hizi za uchovu, nyimbo zilitungwa na kuimbwa wakati shughuli zikiendelea.

Nyimbo hizi ziliimbwa kwa majira na wanaume, wanawake na watoto walioshiriki katika kazi hizo. Nafaka zilizovunwa zilihifadhiwa kwa sehemu iliyoitwa 'Lutsango' au ambayo huwa ni ujenzi ulio juu ya mahali panapopikiwa.

Baada ya kuvuna hasa mahindi, ilikuwa ni kazi ya akina mama kuyatwanga na kusaga ili kupata unga. Wanawake wawili au watatu waliimba kwa zamu na midundo ya kutwanga wakiendeleza shughuli hii. Kila mmoja wa waliotwanga angeweza kuongoza wimbo wenyewe. Waliziimba kurahisisha kazi hasa kutwanga kuondoa makapi na kusaga. Nyimbo hizi zilitwa: 'Maira ga kurima', 'maira ga kuhonda' na 'maira ga kusaga'. Walitwanga wakitumia kinu na mchi.

Mwanamke anayesaga mahindi kati ya mawe mawili (moja juu na moja chini) angeweza kuimba. Jiwe lile la juu huwa na mpini wa mbao uliosaidia kuzungusha hilo jiwe la juu kwa lile la pili (lililo chini) ili kusaga nafaka iwe unga muororo na laini. Kazi hii huandamana na uimbaji wa utaratibu.

Kwa sasa kazi hizi hufanywa na familia ama wengine huajiri wafanyikazi. Jinsi watoto wanavyoendelea kwenda shule, ndivyo wafanyikazi wanazidi kupungua. Kukiwa na kazi nyingi, marafiki na majirani kwa makundi yanayoitwa 'Chikola' (4) hushirikishwa. Nyimbo za kazi za kilimo ni maarufu zaidi kwa wanawake. Hii ndio sababu katika utafiti wetu tumepata nyimbo nyingi zilizoimbwa na wanawake.

Katika sekta ya kilimo, minazi ndio mazao muhimu zaidi ya kiuchumi. Kama tulivyosema, Warabai walijulikana sana kwa ugemaji. Miti hii huendelea kutoa mazao hadi miaka hamsini. Bidhaa zake ni kama: Makuti, madafu, kutengeneza fagio, kuni, vikapu, mikeka ya kulala miongoni mwa nyingine. Ugemaji ni shughuli iliyofanywa na wanaume. 'Mnazi' - pombe ingetumiwa wakati wa tafrija. Waliimba nyimbo zilizoitwa 'Maira ga kujema'.

Utengenezaji wa Makuti

Kazi ya kusuka makuti ya kuezeka nyumba pia ilifanywa na akina mama. Baada ya wanaume au vijana kutoa majani hayo kutoka kwenye minazi, akina mama wangeyasuka aidha kwa

makundi au mtu binafsi. Hata hivyo hatukushuhudia kazi hii kwani siku hizi nyumba nyingi huezekwa kwa mabati.

Ufugaji

Warabai walikuwa wafugaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo. Walitumia ngozi, nyama na maziwa kubadilishana na bidhaa ambazo hawakuwa nazo. Walitumia mifugo hawa kwa

kutolea mahari. Wavulana walipokuwa wakichunga, walikuwa na nyimbo zao, 'Maira ga kurisa'. Pia waliimba walipokamua ng'ombe - 'Maira ga kukama'. Kwa sasa wanaweka mifugo lakini sio kama zamani.

Usasi

Zamani Warabai walikuwa na shughuli hizi za usasi. Wanyama waliowasaka ni kama paa, sungura, ndovu, nyati, tope miongoni mwa wengine. Watu wazima (alume-wanaume) ndio waliofanya kazi hii wakiandamana na vijana. Vijana waliwafuata ili kuwalinda wazee kutokana na hatari za wanyama hawa. Vivyo hivyo waliweza kujifunza usasi kutoka kwa wakubwa wao.

Walitumia njia mbalimbali za usasi. Moja wapo ilikuwa kufuata maburuzo ya nyayo za wanyama hao. Waliweza pia kutumia mbwa walioweza kufuata harufu za wanyama. Mbwa walivishwa kengele miguuni zilizoitwa 'ngamuli". (5)

Wasasi wangeweza pia kutafuta sehemu zenye majimaji ili kutegea wanyama waliokwenda kunywa maji. Waliweza pia kufuata njia za kinyesi cha wanyama hao.

Usasi ulifanywa na wanaume kati ya saba na kumi. Walivishwa hirizi za kuwalinda wasivamiwe na wanyama. Walipomwinda mnyama wangemchinja, wamchune ngozi na wagawanye nyama kati yao. Wakikosa kumpata mnyama ambaye walikuwa wamemfumania kwa mshale, wangetafuta, usaidizi wa 'mganga wa mburuga' ambaye angebashiri upande na sehemu alipoangukia mnyama huyo.

Usasi ulifanywa wakati wa mchana wakati wa kiangazi. Muda wa usasi ungechukua siku moja au hata mwezi mzima. Siku tatu za juma (kuramuka, kurimahiru na kuvisa). Zilikuwa za kwenda shamba, siku ya nne (Jumwa) ilikuwa ya kupumzika na ingeachiwa wasasi.

Waliweza pia kutumia mitego iliyoitwa 'kizina cha muhambo' au handaki. Wangetayarisha handaki katika njia wapitiapo wanyama. Handaki lilikuwa lenye urefu wa mita tano, upana wa mita nne na kina cha mita moja na nusu. Waliweka sumu vijiti vyenye ncha kali katika kina hicho. Halafu mtaro huo ungefinikwa kwa nyasi na kuonekana kama njia ya kawaida. Wanvama waliotegwa katika mahandaki hayo, nyama ilipokatwa, iliwekwa juu ya miti ili ikauke. Nyama hii ilikuja kujulikana kama "nyama ya kuuma na dzua" yaani nyama ya kukauka kwa jua. Walibeba ngozi ambayo ilitumiwa kutengenezea ngoma na mkeka wa kulalia.

Ala za usasi zilirithishwa kwa wawindaji chipukizi. Katika jamii, uwindaji wa muda mrefu ulileta changamoto kwa wanawake walioachwa nyumbani. Walidhulumiwa kimapenzi na wanaume waliokosa kwenda usasini. Mwanamume aliyepatikana na kosa hilo, alifainiwa ng'ombe au 'Malu' ndipo asamehewe makosa yake.

Wakati wa shughuli za uindaji, wawindaji waliimba "Maira ga kuinza" kabla ya kuingia msituni. Siku hizi uindaji umeisha hasa kutokana na serikali kupiga marufuku uwindaji wa wanyama pori. Kwa shughuli hii kwa hivyo hatukushuhudia usasi wowote.

Uchumaji.

Uchumaji wa miti ya misitu ulifanywa kwa njia tatu: Walichuma mizizi, mimea na matunda. Walichuma mizizi kwa matumizi ya chakula na kwa matumizi ya dawa. Mizizi kama *bwere*, *maburu*, *mihogo*, *mzambarao* miongoni mwa mingine. Mizizi uliyotumiwa kama dawa, ilitibu kikohozi, kifua na maumivu ya tumbo. Wazee wa kiume na wa kike ndio waliochuma mizizi hii na waliitumia kutibu watu.

Uchumaji wa mimea au mboga za majani kama vile: *tsalakushe*, *chikosho*, *mnavu*, ulifanywa na wanawake katika ndoa za mitala. Aliyekuwa na jukumu la kupeana mimea au mboga alikuwa ni mke wa kwanza katika boma hilo. Wanawake hao wengine walikuwa na majukumu ya kukusanya kuni, kuteka maji na kupika. Ilikuwa ni mwiko kwa wanawake waliochuma mboga kuzitaja kwa majina kama *mpapayu* na *mtsalafu*. Pia wakati wa kupika, hawakuruhusiwa kupitisha kibanzi cha moto kutoka upande mmoja hadi mwingine. Kama wangesahau kuzingatia mambo hayo, basi iliaminika mboga zilizokuwa zinapikwa zingekuwa uchungu kabisa na kukosa kulika.

Walichuma matunda kama kunazi, mabuyu, makoma, kungu, matonge, maungo, matomoko miongoni mwa mengine. Matunda yalichumwa na vijana waliokuwa wameandamana na wazee walioenda usasini au wakati wa kupeleka mifugo malishoni. Akina mama wangechuna matunda walipokwenda kutafuta kuni. Shughuli hii pia haifanywi kwani matunda, majani na mboga tofauti tofauti huuzwa sokoni. Hatukupata nyimbo za uchumaji.

Uwekaji wa nyuki na uvunaji wa asali.

Warabai pia walipendelea kuweka nyuki na kuvuna asali. Mwanzoni, nyuki walikuwa katika mashimo ndani ya miti mikubwa na wengine walikuwa katika mapango. Baadaye walianza kutengeneza mizinga ambayo si halisi. Hii ilitengenezwa kwa miti ya minazi kwa kuunda mashimo kwenye miti hiyo. Nyuki wangeingia mzinga huo kwa kupitia kwa mwanya mdogo ulioachwa upande mmoja. Halafu walianza kutengeneza mizinga ya masanduku. Mizinga hii ilipakwa dawa za miti shamba na kunyunyiziwa zinguo ili kuilinda. Wakati wa kutengeneza mizinga waliweza kuimba ili kupeana moyo kuendelea na kazi hiyo.

Kila wakati walienda kuangalia kama asali imeanza kuchuruzika. Baada ya muda waliweza kuweka kipindi maalum cha kuvuna asali. Kisadfa walikuja kuamini kuwa wakati wa kuvuna ulikuwa sawa na ule wa kucha za vidole zilivyomea. Kwa hivyo nyuki walipojaa kwenye mzinga, walikata kucha zao. Kucha zilipomea kabisa, walijua asali iko tayari kuvunwa. Ilikuwa muda wa wiki mbili au tatu hivi.

Kabla ya kuchopoa asali, mmoja wa wanaume hao angetafuna aina fulani ya dawa na kuitema kwenye mwanya wa mzinga huo. Waliamini nyuki wote wangetoroka na kuwaachia wavunaji uhuru wa kuvuna asali hiyo. Pia wangechoma moto chini ya mzinga na nyuki wote wangetoroka. Kazi hii yote ilifanywa masaa ya usiku. Wangebonyeza masega ya nyuki ndani ya chombo kilichoitwa 'kithembe'. Halafu wangeichuja iwe nyororo. Wangeigawanya ya matumizi yao na ya kuuza, iliyobaki iliweza kutumika

kutengenezea pombe. Wakati wa shughuli hii ya kuvuna asali hakukuwa na uimbaji wowote. Mazingira yalihitajika kuwa tulivu ili wasiumwe na nyuki hao.

Shughuli hii ya uvunaji wa asali haifanywi kama zamani. Weledi wa kazi hii walistaafu na kuingilia zaidi ugemaji wa pombe ya mnazi. Uchumaji wa mizizi umeachiwa wazee wa kiume na wa kike ambao ni wataalamu wa mitishamba na waganga. Hii ni shughuli muhimu hasa kutokana na imani inayohusu uchawi.

Ufumaji wa vikapu na mikeka

Kazi hii ilifanywa na wanawake makamo. Wakati mwingine walisaidiwa na mabinti kazi ilipokuwa nyingi zaidi. Walisuka vikapu na mikeka wakitumia mikonge. Walibadilishana bidhaa hizi na jamiii ya wakamba. Kazi hii iliachwa zamani wakati ubadilishanaji wa bidhaa ulipokoma.

Uvuaji wa samaki

Warabai pia waliweza kujishughulisha na uvuaji wa samaki kama kitega-uchumi. Waliweza kuvua ufuoni mwa Bahari Hindi. Walipata kitoweo kutokana na samaki waliowavua na walipokuwa wengi waliweza kuwauza kwa hoteli zilizoko kando kando mwa pwani hiyo.

Hitimisho

Tumeonyesha shughuli na kazi tofauti tofauti zilizofanywa na Warabai, kwani nikupitia kazi hizo ndio tungebainisha kama ziliendelezwa kwa matumizi ya nyimbo au la.

Tanbihi.

1. Jina Rabai kutokana na “Raha ii” likaja kuwa ‘Rahai’ sasa Rabai. Haya ni maelezo kutoka kwa babu Chengo.

Maelezo haya yalitolewa na Wedzuware na Mdaro tarehe 10/3/2012

2. Kambi-Inaweza kufananishwa na mahakama ya leo ambapo wazee walisuluhisha ugomvi wowote katika jamii
3. Nyimbo za oma: maelezo kuhusu aina mbali mbali za ngoma yalitolewa na bibi Mkambe na mzee Ndaro tarehe 20/4/2011
4. Chikola: marafiki na majirani wanaoshirikishwa katika shughuli mbalimbali za kazi na hasa ‘kilimo’
5. Ngamuli- kengele zilizoovishwa mbwa miguuni. Maelezo haya yalitolewa na Baya Washe

SURA YA TATU:

MBINU ZA KIMTINDO KATIKA NYIMBO ZA KAZI ZA JAMII YA WARABAI.

3.0. Utangulizi:

Sura hii inachanganua mbinu za kimtindo katika nyimbo teule za kazi za jamii ya Warabai. Lengo kuu la sura hii ni kuelewa uwezo wa habari inavyopashwa kupitia nyimbo ambazo tulizishughulikia.

Katika sura hii, sehemu ya kwanza tumefafanua baadhi ya mbinu za kimtindo na tamathali za semi (lugha). Sehemu ya pili tumeeleza maudhui pamoja na jinsi mitindo na tamathali za semi zilivyojitokeza katika nyimbo zilizochanganuliwa.

Lugha ni muhimu sana kwa kazi yoyote ile ya fasihi. Kwa mujibu wa Ryanga (2006), mtunzi wa kazi ya kisanaa hujishughulisha na taathira za lugha kwa hadhira lengwa, hivyo kuboresha umbo na lugha anayoitumia. Anaendelea kusema, ufanisi huu ni zaidi kwa msanii wa fasihi simulizi kwa sababu sanaa haiwezi kuendelezwa kimapokezi kama si lugha inayochangamsha na kuwafanya watu waikumbuke. Anaonyesha kuwa kitamaduni, mwimbaji mweledi huwa na ukwasi wa lugha na ujuzi wa tamathali za semi.

Vile vile Ryanga akimnukuu Saussure (Halliday 1978) anaendelea kusema, lugha ni Suala la kijamii. Fasihi simulizi huibuka kutokana na chemchemi za fikra ama moyo wa msanii na hujitokeza kwa kutumia chombo cha lugha ambayo husaidia kueleza undani wa hisia na mguso wa mwimbaji kutokana na tajriba za jamii. Mwingine anayezungumzia matumizi ya lugha katika fasihi simulizi ni Shitemi (2006) ambaye anasema masimulizi

ya kidegesturi kupitia nyimbo na hadithi zenye asili katika matukio ya kihistoria, huhusisha lugha. Misemo, jazanda, vitanza ndimi na tanakakali za sauti hunasa na kuzungumzia miktadha mbalimbali ya maisha. Anaendelea kusema fasihi simulizi ni sanaa inayotumia lugha kama malighafi.

Mahali pia huweza kuathiri lugha katika kazi yoyote ya kisanaa. Kama asemavyo Ngara (1981), kuwa mahali hudhihirisha au kuathiri sanaa ya uchaguzi wa lugha. Wazo hili linaonyesha ukweli wa elimu ya lugha kuwa sio utaratibu wa ishara zenye maana bali uhalisi wa mfano wa thamani, mwelekeo, hulka na desturi kwa jamii anayoitumia.

Ngara akimnukuu Pratt na Traugott (1980) anasema;

”Lugha hutumiwa kutekeleza matumizi ya kupitisha habari zenye maana kutoka kwa mnenaji hadi kwa hadhira (kutoka mwimbaji hadi kwa msikilizaji) kwa kusudi la kupata walengwa kutenda mambo yanayotakikana au kubadili mienendo ya wasikilizaji (waimbaji) hao.”

(Tafsiri yetu)

Kwa mujibu wa Wamitila (2004), akizungumzia matumizi ya lugha, anazingatia tamathali za semi katika tashbihi, misemo, takriri, jazanda, istiari na tanakali za sauti. Anasema mtindo ni jumla ya mbinu au sifa zinazomwezesha kuwasilisha ujumbe wake. Ni jinsi au namna ya kufanya kitu kwa kuzingatia misingi fulani. Yaani ni jinsi kitu

kinavyoelezwa kwa mfano; kwa kutia chumvi, kwa kuuliza maswali, kejeli, kinaya, uhuishaji, miundo ya sentensi, msamiati miongoni mwa nyingine.

Wahakiki wengine wa kazi za fasihi kama Waititu na Oyugi (2005), Aregi (2005), Njihia (1990), na Matti (2003) wameeleza matumizi ya lugha na mbinu za kimtindo au za sanaa kwa njia isiyo na utofauti mkubwa. Yaani wameeleza matumizi ya lugha na mbinu za kimtindo bila kuonyesha mipaka yoyote.

Ni wazi kuwa kuna mpaka finyu sana katika kutizama matumizi ya lugha na mbinu za kimtindo au za kisanaa. Baadhi ya tamathali za semi kama methali na semi huwa na maana fiche na mbinu za kimtindo kama tanakali za sauti, takriri, huwa hazina maana fiche au maana ya ndani.

3.1 Uchanganuzi wa nyimbo za kazi

Katika kubainisha mbinu za kimtindo, tumejadili pia maudhui kwa ufupi ili tupate msingi wa kuelezea mbinu zilizotumika kuyawasilisha maudhui hayo. Kama asemavyo Wamitila (2008), maudhui yana uhusiano mkubwa na mtindo. Ni kupitia mtindo ambapo msanii huweza kuwasilisha maudhui yake. Ubunifu wa mtunzi na uwezo wake wa kuteua mbinu mwafaka ndivyo vifaa vinavyomwezesha kuwasilisha ujumbe wake.

3.2 Juhudi katika kazi

Maudhui ya kwanza ni juhudi kazini. Mwafrika kwa jumla huithamini juhudi katika kazi na kudharau wazembe. Kuna nyimbo kadhaa ambazo huimbwa wanajamii wanapolima, wanapotwanga, wanaposaga au hata kupepeta. Nyingi za kazi hizi hufanywa na akina

mama na mabinti wao. Lengo huwa ni kutiana shime katika kazi ili waifurahie na kuirahisisha kazi hiyo.

Nyimbo nyingine ziliimbwa na mabinti walioachwa nyumbani wakati mama alikwenda shughuli za matanga au harusi. Wasichana wangepokezana wakitwanga. Walijizatiti kufanya kazi ya kutwanga na kusaga ili wasiadhibiwe na baba zao.

Nyimbo zenyewe zilisisitiza umuhimu wa kusaga nafaka kama vile mahindi na muwele ili waweze kupata chakula. Ilikuwa ni hatia kupata mgeni au jamaa anapotembea, akose kuandaliwa chakula. kwa mfano katika wimbo wa kusaga.

Ifuatayo ni mifano mbinu za kimtindo katika nyimbo za kazi za jamii ya Warabai.

Sentensi fupi

Sentensi ya wimbo inapokuwa na neno moja, mawili au matatu husemekana na wataalam wa kimtindo ni sentensi fupi. Huwa na lengo la kuwasilisha ujumbe fulani kwa maksudi maalum. Mara nyingi hubeba hoja moja. Sentensi fupi huwa na sifa ya kufanya mtitimo unaokwenda upesi upesi. Sentensi hizi pia huleta mdundo katika wimbo. Mohammed (1995) anasema:

“Sentensi fupi fupi hutumika kujenga taathira ya utendaji na kwamba sentensi hizi huweka makato ya mikazo, mipando na mishuko ya sauti yenye vipimo vya masafa mafupi na hili husababisha sehemu hiyo kusikika au kusomeka kwa mtitimo wa haraka.”

Kwa mfano, katika wimbo wa “Natwanga”

Natwanga, natwanga,

Kisha nisage.

ya baba sitayaweza,

mama anakuja kesho,

kesho machweo.

Lengo hapa ni kusisitiza kutwanga ili kutayarisha chakula kabla ya baba kufika nyumbani

Pia katika wimbo kutwanga na kusaga,

watu hutwanga, wakasaga.

sageni, sageni mje tule.

mamake Ngolo, hee! hee!

x2

Katika kifungu hiki wimbo umeendelezwa kwa sentensi zenye maneno yasiyozidi manne kwa kila mstari. Ujumbe ni mmoja, kule kutwanga na kusaga.

Ufupi wa sentensi zenyewe huwa ni midundo inayoandamana na kazi inayofanyika. Kwa mfano;

Nina mgeni wangu ee,

halali na njaa.

mamake mwaka wee,

saga unipe hilo jiwe.

Katika wimbo wa 'kupepeta' sentensi pia ni fupi fupi kwani kazi hii hufanywa kwa haraka haraka.

Kadzo pepeta pepeta mtama - } kiongozi

Kadzo pepeta pepeta - } wote

Ujumbe unaotolewa hapa ni mfupi ule wa kupepeta mtama.

Takriri

Neno linarudiwarudiwa ili kupata umbo moja. Ni maneno au mstari unaorudiwarudiwa katika uimbaji. Msokile (1993) anasema, ni marudio ya neno, sauti, herufi au wazo na kadhalika katika kazi ya sanaa ya kifasihi. Naye Ngure (2003) anaeleza takriri kama ule urudiaji wa silabi au sauti zinazolingana katika maneno yanayokaribiana kimatamshi.

Kwa mfano; katika wimbo wa 'kulima,'

Jembe, ee jembe makinika } x2
Watu wakilima. }

Neno jembe limerudiwa mara mbili kuisisitiza ndicho kifaa kinachotumika kwa kazi ya kulima. katika wimbo wa 'natwanga'.

Natwanga, natwanga.

kisha nisage.

Neno 'natwanga' pia limerudiwa mara mbili. Pia urudiaji huu unalenga kuwatia shime wahusika, waweze kuendelea na kazi yao vizuri. Mara nyingi urudiaji huu huwa katika kiitikio.

Nidaa

Mbinu hii pia huitwa siyahi. Ni matumizi ya kauli za kuajibia. Mbinu hii inaelezwa na Kuhenga (1977) kama;

“Namna ya msemu wa msimuo au sauti ya mshangao atoayo mtu kudhihirisha maoni yake ya ndani au kilio cha moyo wakati apatwapo na mgutusho ghafla wa furaha, hasira, huzuni, chuki au mshtuko wowote wa moyo”

Katika uimbaji, mbinu hii mara nyingi hutumiwa kuonyesha hisia za ndani za mwimbaji. Matumizi yake humfanya msikilizaji (na mwimbaji mwenyewe) kushiriki kihisia na kimaono katika uimbaji huo. Katika wimbo wa 'kutwanga na kusaga,'

Mamake Ngolo, hee! Hee!

Nidaa hapa imetumika kuleta hali ya kuondoa uchovu kwa wafanyikazi hawa.

Katika wimbo wa 'kusaga', vifungu vyote vinaanza na nidaa.

“Nina mgeni wangu ee!

halali na njaa

Nina mkwe wangu ee!

Halali na njaa

Nina mtoto wangu ee!

Halali na njaa

Hapa siyahi imetumika kuonyesha hisia za furaha iliyochanganyika na hofu ya kutojua kama kweli atapata anachohitaji kutoka kwa mhusika mwenzake.

Balagha

Kulingana na kamusi kamili ya Kiswahili (2009), balagha ni ufundi wa matumizi ya lugha kwa nia ya kumfanya msikilizaji ashawishike au afurahi. Swali la balagha ni swali lisilohitaji jibu linaloulizwa kwa nia ya kusisitiza. Msokile (1993) anaiita mbinu ya tashtiti. Anasema ni matumizi ya maswali ambayo majibu yake kwa kawaida yanakuwa yameeleweka.

Swali hilo linakuwa kwa ajili ya msisitizo tu au mshangao. Katika wimbo wa ‘kulima, kutwanga na kusaga’ mbinu hii imejitokeza vizuri.

1. Jembe, ee jembe makinika, } x2 kiongozi
watu wakilima. }

wanalima vipi?
nami nikalime vivyo hivyo. } x2 wote

2. Kinu, ee kinu makinika,
watu wakitwanga. } x2 kiongozi

wanatwanga vipi?
nami nikatwange vivyo hivyo. } x2 wote

3. Jiwe la kusaga, ee makinika,
watu wakisaga, } x2 kiongozi

wanasaga vipi?
nami nikasage vivyo hivyo. } x2 wote

Wimbo mzima umejaa maswali ya balagha. Ni wazi kwamba hatutarajii majibu kutoka kwa vifaa hivyo. Lengo ni kutiana shime ya kuendelea kulima, kutwanga au kusaga kwa kutumia vifaa husika.

Chuku

Ni mbinu ya kutilia chumvi-jambo ili kuonyesha uziada wa jambo. Katika Kamusi fafanuzi ya Misemo (2011) inasema chuku hutumiwa hasa wakati mtunzi anapoashiria mshangao au anapotaka kukuza jambo dogo kupita kiasi. Wambua(2001) ameorodhesha aina tatu za matumizi ya chuku kama vile:

1. Kuonyesha jambo la kustaajibisha.

2. Jambo kubwa kukuzwa kupita kiasi.
3. Jambo dogo kudunishwa kupita kiasi.

Katika wimbo 'natwanga', mwimbaji anatumia chuku akielezea woga alio nao kwa mzazi wake wa kiume. Chuku hii imeelezwa kwa msemu, 'ya baba sitayaweza' ikiwa na maana kuwa asipokutwa ametayarisha chakula huenda akaangukiwa na ghadhabu ya baba yake, jambo ambalo analiona zito na ndio anasema 'hatayaweza.'

Tashihisi

Tashihisi ni usemi wenye kukipa kitu kisicho na uhai sifa ya kitu chenye uhai. Yaani ni kuvipa sifa za binadamu na kuonekana kutenda kama binadamu. Hii ni kwa mujibu wa Kamusi Kamili ya Kiswahili (2009).

Kwa mfano;

1. Mlango ukamkodolea macho mgeni.
2. Maua yote bustanini yalishangilia kwa kupiga makofi.
3. Baada ya kulia kwa muda mrefu, usingizi ulimhurumia na ukamchukua.

Katika wimbo wa 'kulima, kutwanga na kusaga,' ni kama waimbaji wanazungumzia zana hizi za kazi, zielezee jinsi watu wanavyozitumia. Kifungu cha kwanza, jembe linatakikana lielezee watu jinsi linavyolima. Kifungu cha pili, kinu kinatakikana kieleze jinsi kinavyotumiwa kutwanga nafaka. Kifungu cha mwisho jiwe la kusaga "lwala"

linasihiwa lieleze watu jinsi linavyotumika kusaga nafaka mbali mbali. Vifaa hivi vitatu vimepewa sifa za kuzungumza kama binadamu.

Katika kusisitiza faida za kupepete kadzo anaambiwa;

“Na njaa isijione!”

Kauli hii ni uhuishaji. Kwa kawaida binadamu ndiye huhisi njaa na sio njaa kujiona. Kuona kunahitaji macho na ni kitendo kinachoweza kufanywa na binadamu tu au mnyama

3.3 Ufugaji

Hapa tutaangalia nyimbo zinazohusiana na ufugaji. Tumetangulia kueleza katika sura ya pili kuwa kazi ya ufugaji ilifanywa na vijana wa kiume na wakati mwingine wazee wa makamo. Waliimba nyimbo hizi kupitisha wakati wakisimamia mifugo wakiwa malishoni.

Nyimbo hizo zilidhihirisha kulalamika kwa mchungaji kuwa anafanya kazi ngumu kuwapeleka ng'ombe malishoni lakini hafurahii kunywa maziwa ya ng'ombe hawa. Kutokana na mahitaji mengi ya kijamii, ng'ombe walifugwa kwa madhumuni ya kuuza maziwa. Kwa mfano, wimbo wa 'mchungaji wangu.'

Baadhi ya nyimbo hizi zimeelezea kazi ya kuwalisha mifugo. Kazi hii inahusu kuwachukua mifugo asubuhi, kuwapeleka malishoni, kuwasimamia na kuwarudisha jioni. Kwa mfano, wimbo wa 'kuchunga'.

Nyimbo nyingine za ufugaji zimeonyesha jinsi wafugaji wanavyokubaliana na maendeleo ya matumizi ya kisayansi katika ufugaji wao. Walipoelimishwa kuwa mifugo huhitaji kuangaliwa vizuri kama kuwapa dawa za minyoo, kudungwa sindano na lishe bora, waliridhishwa na mambo hayo. Walikubaliana na masomo yanayotolewa na daktari wa mifigo. Mfano ni wimbo “nikamdunge ng’ombe wangu”.

Mbinu za kimtindo katika nyimbo hizi ni kama:

Sentensi Tongole

Hizi ni sentensi au maneno ambayo huwa yanasemwa katika wimbo badala ya kuimbwa kwa mdundo uliomo katika wimbo husika. Hii ni kwa mujibu wa Mohammed (1995). Katika wimbo ‘Mchungaji wangu’ kiongozi wa wimbo anatamka maneno fulani katika wimbo bila kuyaimba.

Mchungaji wangu ee, }
mchungaji wangu aa. } kiongozi

Mchungaji wangu wee, }
hanywi maziwa. } wote

nitamwambia baba - kiongozi

Maneno “nitamwambia baba” huwa hayaimbwi bali yanatamkwa tu na kiongozi.

Tashbihi

Ni usemi unaofananisha kitu kimoja na kingine kwa kutumia maneno kama vile mithili ya, kama, sawa na, au na mfano wa, kwa mujibu wa Msokile(1993).

Ifuatayo ni mifano ya tashbihi:

1. Fatuma ni mweupe kama bafta.
2. Daudi alifoka kwa hasira mithili ya simba.
3. Alitembea taratibu mfano wa malaika.

Katika wimbo wa 'mchungaji wangu', mtunzi ametumia tashbihi mara mbili. Kwanza anafananisha kazi yake kuwa ni kubwa au ngumu 'kama ndovu'. Pili, japo kazi hii ni ya kuchosha kwa ugumu wake, malaji ya mchungaji ni 'kama chungu'. Kwa ujumla mchungaji anaona kazi yake haimfaidi yeye binafsi'.

Sentensi fupi na ndefu

Sentensi ndefu hutokea pale wimbo unapokuwa na maneno zaidi ya manne katika sentensi. Kuna aina mbili za sentensi ndefu yaani ambatano na changamano. Mohammed (1995) anasema kwamba:

“Sentensi ndefu ndefu zinapunguza mwendo wa mtitimo na hivyo kumfanya msomaji (msikilizaji) adodee anaposikiliza kwa utaratibu huo”.

(Tafsiri yetu)

Sentensi ndefu zimetumika kutoa maelezo fulani katika wimbo. Huweza kuwasilisha ujumbe wenye huzuni, uvivu ama wenye kuonyesha hali ya kukinai. Sentensi hizi huweza kusheheni maudhui mengi.

Katika wimbo wa 'kuchunga' sentensi ndefu zimetumika. Hii ni kwa sababu wimbo umesheheni mawazo mazito ya hatua zinazochukuliwa kwa kazi hii ya ufugaji. Ni ndefu kwani anaelezea kazi inavyofanywa kutoka asubuhi hadi jioni.

“Unawatoa asubuhi, ikifika jioni,

Unawarudisha wapumzike.

Unawarudisha nyumbaninwapumzike hadi kesho.

Hao mbuzi, kondoo na ng'ombe.

Sentensi fupi

Katika nyimbo hizi pia kuna matumizi ya sentensi fupi.

Mchungaji wangu wee!
hanywi maziwa. } x2

Katika wimbo, 'Nikamdunge ng'ombe wangu amejadili umuhimu wa matumizi ya sindano au mbinu za kisayansi za ufugaji ili kupata faida. Kila mstari wa wimbo huu una maneno mawili au matatu tu.

Nifungulie mlango,

na sitaki oungo,

daktari nataka sindano,

nikamdunge ng'ombe wangu. x2

Urudiaji

Karibu nyimbo zote za ufugaji zina mbinu hii ya takriri. Kuna urudiaji wa neno 'mchungaji,' kuonyesha ndiye mhusika mkuu wa kazi hiyo ya ufugaji. Maneno 'hanywi maziwa' yanatilia mkazo wazo kuwa japo anafanya kazi hiyo ya kuwapeleka ng'ombe malishoni katu hapati fursa ya kuyanywa maziwa kwani yanauzwa yote.

Katika wimbo 'kuchunga' neno 'natuchunge' limerudiwarudiwa kutilia mkazo kazi ile ya kuchunga. Mstari 'watakuja kuokoa' pia limerudiwa kuonyesha sio kazi ya bure bali ina faida kwa wakati wake.

Kiitikio: natuchunge, natuchunge, x2- kiongozi

Watakuja kuokoa. x2 – wote

Misemo

Ni tamathali ya usemi ambapo ukweli hufupishwa na kuwekwa katika maneno machache.

Msokile (1993; 44) akifafanua misemo anasema:

“Matumizi yake katika fasihi ni lazima yategemee uhai wake katika matumizi yake ya kwawaida katika jamii”.

Hujengwa kwa kutumia maneno ya kawaida lakini yaliyoficha maana tofauti na ile iliyobebwa na maneno yaliyotumika. Kwa mfano;

1. Jakobo amekata Kamba (amekufa).
2. Iva uso (kuona haya).
3. Kaza roho (kuvumilia mambo magumu).

Katika wimbo 'nikamdunge ng'ombe wangu' kifungu 'nifungulie mlango' hakina dhana ya moja kwa moja kuwa anataka kuingia nyumbani. Hii ni kauli ya kumtaka mtu amakinike, akusikilize na kukutimizia yale unayohitaji. Anataka daktari ampe sindano ya kundunga ng'ombe wake.

Msemu wa pili unapatikana katika kifungu 'mchungaji huenda na moja'. Kifungu hiki kina maana kuwa ameamua kazi yake ni ufugaji na hatahitaji kujihusisha na mambo mengine ambayo yanaweza kumfanya asifaidike kwa shughuli za ufugaji.

Jazanda

Mohammed (1986) ameeleza jazanda kuwa ni mbinu ya kupatia kitu jina la kitu kingine ambacho kinafanana nacho kwa sura, tabia au sifa ingine yoyote. Jazanda ni matumizi ya lugha kimaumbo kwa kuipa dhana maana iliyo mbali na maana ya kawaida. Mwanzia (2007), akimnukuu Ngure (2003: 1631) anaelezea jazanda kama lugha inayochora picha ya mahali au vitu kwa kutumia tamathali za usemi. Kwa mfano; kutaja 'jembe' ukiwa na maana ya kuwaambia watu waanze kazi ya kulima.

Neno 'kuokoa' limetumika kijazanda katika wimbo wa 'kuchunga'. Mtunzi anazungumzia kuhusu mifugo kama wakombozi kwa sababu ya faida chungu nzima wanazopata kama maziwa au pesa wanapouza mifugo hawa. Kwa hivyo badala ya kulitaja neno 'faida' ameleta fumbo hilo kuwa ni kama wakombozi wanaokuja 'kuwaokoa' au kwasaidia maishani.

Uteuzi wa msamiati

Uteuzi wa msamiati katika kazi ya sanaa huwa ndio kiini cha mtindo ili kuwezesha ujumbe kufikia walengwa.

Msamiati ni jumla ya maneno katika lugha fulani. Maneno yote katika matini fulani (nyimbo) huwa ni msamiati. Haya ni kwa mujibu wa TUKI (2004:272). Kuna msamiati mgumu au teule na msamiati wa kawaida ule unatumika na wanajamii kama wa kimapokeo. Kunaweza kuzuka msamiati wa msimu ambapo maneno mapya huzaliwa na muktadha na mazingira maalum.

Msamiati huu huweza kupotea baada ya kipindi fulani au ukatumika kwa muda mrefu na kukubaliwa kama msamiati wa kawaida.

Katika nyimbo hizi za ufugaji kuna maneno kadhaa ambayo yameendelezwa kama ya Kiswahili na ni ya Kirabai. Hii inadhihirisha ukuruba uliopo kati ya lugha ya Kiswahili na ile ya Kirabai. Maneno yenyewe ni aina ya mifugo kama; ng'ombe, mbuzi, kondoo. Pia maneno kama sindano, daktari, na fisi ni msamiati sawa na wa Kiswahili. Kuna uwezekano mkubwa kuwa Warabai wamekopa msamiati huu kutoka kwa Waswahili.

Methali

Methali ni usemi wa kisanii wa kimapokeo unaofikiriwa na jamii kuwa kweli na unaotumiwa kufumbia au kupigia mfano na huwa umebeba maana pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa. Kamusi ya Kiswahili Sanifu(2010).

Methali hutumia maneno kimapokeo. Kwa kawaida mafungu ya maneno hayo huwa ya busara.

Hekima hiyo hutegemea mukhtadha hali ambapo methali hutumika. Kwa mujibu wa Kinge'i (1982:uk.29) methali huanza kama msembo wa kawaida na ambao kwa mvuto wa ufasaha wake hupewa wajibu mkubwa na umashuhuri na kutokana na marudio ya matumizi yake hutokea kuhesabiwa ama kukubalika kama methali, kwa mfano;

1. Mchagua jembe si mkulima.
2. Mgema akisifiwa tembo hilitia maji.
3. Kitema kuni temato.

Katika wimbo wa “nikamdungè ng’ombe wangu” kauli “mbili zilimshinda fisi” ni sehemu ya methali ambayo kwa ukamilifu inasema, “njia mbili zilimshinda fisi.” Mwindaji anaeleza kuwa ameamua kazi yake ni ufugaji na ataizingatia vilivyo ili awe na ufanisi wa hali ya juu. Hataki kujisumbua na shughuli nyingi za kazi tofauti zitakazomfanya akose kumakinika kwa mifugo wake.

3.4 Ugemaji.

Kazi nyingine ambayo inachukua nafasi kubwa katika maisha ya Warabai ni ugemaji. Kazi hii ilifanywa na akina baba na wakati mwingine vijana wa makamo walihusishwa pia ili warithishwe kazi zenyewe. Walijihimiza katika kazi hii kupitia nyimbo.

Baadhi ya nyimbo zilisifu faida ya kazi ya ugemaji. Zilieleza hatua ya jinsi pombe hasa ya 'mnazi' inavyogemwa, kwa mfano; katika wimbo 'kugema' mtunzi anatwambia mgema hupanda mnazi baada ya kuweka makali kisu maalumu cha ugemaji (luhumba). Anapanda tagaa akiwa na aina fulani ya kibuyu cha kutegea tembo lenyewe. Tembo likiwa tayari linauzwa na anapata faida ya pesa.

Nyimbo za ugemaji ziliimbwa hata wakati wa siasa. Kwa mfano, miaka ya themanini kulikuwa na tisho la kutaka kupiga marufuku utengenezaji na unywaji wa pombe ya 'mnazi'. Wanajamii pamoja na wabunge kadhaa kama marehemu Karisa Maitha na Mbunge Chibule wa Tsuma walikuwa mstari wa mbele kupinga jambo hili.

Nyimbo ziliwahimiza wabunge au wanaotaka kuchaguliwa, kuwa hawana budi kutetea maslahi ya wagama. Wanajamii wengi waliweza kusomesha watoto wao kwa uuzaji wa 'mnazi' kwa mfano; 'wimbo wa ugemaji'.

Mbinu za kimindo zilizotumika katika nyimbo hizi ni kama:

Sentensi:

Kuna mchanganyiko wa sentensi sahili na sentensi changamano. Pale ambapo ni fupi; hueleza jambo au wazo moja kwa uwazi, kwa mfano katika wimbo, 'ugemaji', mistari miwili ya kwanza, anataka mbunge amakinike na asikize kile wanachotaka kumwambia,

Mbunge wetu Chibule,

tunataka kujua.

uchaguzi ambao unakuja,

tunataka urudi bunge mwenzetu.

uweze kujua sisi tunanyang'anywa.

Mistari miwili ya mwisho ambayo ni sentensi ndefu, inadhihirisha uzito wa mawazo. Wanataka kumjulisha mbunge wao kama akitaka kuchaguliwa tena, lazima ashughulikie maslahi ya wanajamii. Afahamu ana jukumu la kutekeleza nalo ni kuwatetea wagama waendeleo na kazi yao.

Takriri

Neno faida limerudiwa tena kwa njia ya kulivuta, katika wimbo huu wa 'kugema'. Madhumuni ya kulivuta neno hili ni kusisitiza faida inayopatikana kutoka kwa mnazi hasa kupitia kazi ya ugemaji.

Kugema kuna faidaa,

kazi ya kugema aa,

kugema kuna faida.

Pia kuna urudiaji wa neno 'mgema' katika wimbo wa 'ugemaji'. Linasisitiza ndiye anayetakikana kujua matatizo ya wanajamii. Neno 'analia' vile vile limerudiwa kutilia mkazo huzuni walionayo wagema na hata wale wanaogemewa, ikiwa uuzaji wa 'mnazi' utakomeshwa

Mgema, mgema analia,

anayegemewa pia analia,

twendeni kwa Chibule,

ndiye atotuokoa.

Tashibih

Faida na uzuri wa kazi ya kugema na mnazi wenyewe, inasemekana kuwa na utamu ambao unafananishwa a asali ya nyuki; kama ilivyo katika wimbo wa 'kugema'.

Una kazi nzuri,

una utamu wake,

kama asali ya nyuki.

Msamiati

Maneno kadhaa yamekopwa moja kwa moja kama yanavyoendelezwa kwa lugha ya Kiswahili. Maneno hayo ni mbunge, mnazi, asali na neno faida.

3.5 Ujenzi wa nyumba

Kazi hii ilifanywa na mabarobaro wa kijiji husika. Wazee kadhaa wangeweza kusaidia lakini jukumu kuu lilikuwa ni la vijana. Waliungana na kujenga kwa mwana jamii aliyehitaji usaidizi huu.

Katika nyimbo hizo waliweza kueleza mambo muhimu katika ujenzi wa nyumba. Walijikumbusha kuwa nyumba huweza kujengwa kwa miti na nyingine kwa mawe. Katika nyimbo zingine wanataja vifaa muhimu vya kutumiwa kama fito, misumari, mabati au makuti. Wangeeleza baadhi ya hatua muhimu za ujenzi kama kuchimba mashimo ya msingi, kuweka fito au mawe, kuipandisha na kuiezeka aidha kwa makuti au mabati.

Baadhi ya mbinu za kisanaa na matumizi ya lugha zilizotumika ni;

Sentensi

Katika nyimbo hizi kuna aina tatu za sentensi; fupi, ndefu na tongole. Sentensi fupi zimetumika kueleza na kusesitiza wazo moja kama 'ukitaka kujenga'. Sentensi ndefu zimeelezea hoja nzito yaani kuelezea hatua za ujenzi wa nyumba. Sentensi tongole imetumika katika wimbo huo huo wa ujenzi wa nyumba. Mtunzi anauliza kama nyumba iko tayari kwa hali ya kusema bila kuimba katika mstari 'Hiyo nyumba imeiva'.

Balagha

Wimbo wa ujenzi wa nyumba pia umetumia swali la balagha, baada ya kila kifungu. Swali hilo haliimbwi bali linatamkwa tu na kiongozi wa wimbo. Baada ya kutaja hatua fulani za ujenzi anauliza', je, hiyo nyumba iko tayari?' Hili ni swali lisilohitaji jibu la moja kwa moja kwani nyumba huhitaji mambo mengi kama kukandikwa kwa udongo, kuweka fanicha na vyombo anuai, ili mja aweze kusema kweli nyumba inastahili kuwa makao ya binadamu.

Mtu akitaka kujenga. x 2 kiongozi

Hutumia miti au mawe,
huchimba mashimo ya msingi,
ndio aweze kupandisha juu. } wote

Hiyo nyumba imeiva? - Kiongozi

Msemo

Katika kila swali la balagha la wimbo wa ujenzi, kuna msemo ambao umejitokeza. Kifungu, 'nyumba imeiva?' neno 'kuiva' kwa kawaida ni kusema chakula kiko tayari. Kifungu hiki kinā maana ya kuuliza je, hiyo nyumba iko tayari na watu wanaweza kufanya makao yao hapo? Usemi huu unadhamiria kuwahimiza wajenzi kufanya kazi na kuikamilisha bila ulegevu wowote.

3.6 Mawaidha ya kazi

Finnegan (1970) anaeleza kwamba fasihi simulizi hutumiwa kuukuza ushirikiano kuwaleta watu (wanajamii) pamoja. Wakati mwingine wazee na akina mama hupitisha wakati wao masaa ya jioni (hasa wakati wa mbalamwezi) kushauriana kuhusu umuhimu wa kazi. Waliweza kuimba nyimbo za kuwakosoa wanajamii walioonekana kuzembea katika kazi mbali mbali. Nyimbo zenyewe ziligusia kazi tofauti tofauti.

Baadhi ya nyimbo zilizokuwa zinatoa mawaidha, ziliashiria jinsi wazee Warabai walivyochukizwa na majilio ya wamishonari katika maeneo yao. Walihofia maisha yao huenda yakabadilishwa. Walitunga nyimbo ambazo ziliwashauri watoto wao na vijana, wasipendeleo sana kushirikiana na wageni (wamishonari) ambao kwa maoni yao waliona hawajui kazi za kulima au hata kugema (kazi ambayo walienzi sana kama asemavyo Spear (1948) kwa mfano wimbo 'Warabai'.

Nyimbo zingine zilikosoa uvivu na kuwashauri wanajamii kuwa watu wa bidii kazini. Mfano mzuri ni wimbo wa 'mtu mvivu' na 'nataka wa kazi'.

Baadhi ya mbinu za kisanaa katika nyimbo hizi ni:

Kejeli

Tamathali hii hutumia maneno ambayo kwa kawaida huwa ni kinyume kabisa na maana inayotarajiwa kutoka kwa maneno hayo. Kulingana na Ruo (1989), kejeli au kinaya ni tamathali ya semi ambayo hukusudiwa. Kuna uwezekano wa kumsifu mtu fulani kuwa ni nadhifu wakati ni mchafu au kuonyesha jinsi alivyo karimu kumbe ni bahili.

Katika wimbo 'Warabai' wanawakejeli wamishonari kuwa hawajui chochote ila kutembea tu. Hii ni kinaya na pia kuwadunisha kwani haimaanishi wamishonari hawa hawakujua au hawakufanya kazi yoyote ile.

Akina baba, akina mama, Warabai,

huzungumza na kusema,

wamisheni hawagemi, hawalimi,

kazi yao ni kutembea.

Urudiaji

Nyimbo hizi za mawaidha ya kazi pia zina urudiaji wa maneno zinapoimbwa. Neno 'ngoma' katika wimbo 'mtu mvivu' limerudiwa mara tatu kwa kila kifungu ili kumwezesha yule mhusika mvivu kujua anahitajika kujiunga na wengine kufanya kazi katika jamii. Neno 'rafiki' na 'mwenzangu' pia limerudiwarudiwa kuisisitiza umoja walionao na kwamba hawangependa yeyote awe na uzembe katika jamii yao.

Katika wimbo 'nataka wa kazi' maneno haya yamerudiwa mara mbili katika kila kifungu kutilia mkazo kuwa hana haja ya mume mvivu. Neno 'shangazi' limekaririwa kumsisitizia shangaziye kwamba afanye uchunguzi wa kutosha kwa mchumba anayemtafuta ili apate mtu atakayeweza kuyakimu maisha yake kupitia juhudi zake za kazi.

Naupanda juu ya mlima huo mgomba,

natakaa mwenye kazi shangazi,x2

ambaye hana kazi atanipa nini?

shangazi nataka mwenye kazi.

Vivyo hivyo kuna urudiaji wa neno 'usiende' katika wimbo wa 'Warabai'. Lengo ni kuwasisitiza watoto na vijana wasifuate mambo ya wamishonari kwani watashindwa kufanya kazi zao muhimu kama kugema na kulima.

Wimbo wa 'kazi anuai' maneno, 'Haya wee!' ambayo ni nidaa pia yamerudiwarudiwa kwa kila kifungu, kutilia mkazo jinsi walengwa wanavyotakikana kisikiliza ujumbe huo kuhusu kazi. Kifugu 'kazi ni leo' kimerudiwarudiwa kila baada ya mstari mmoja. Lengo ni kusisitiza kuwa kazi lazima zifanywe kila wakati na hakuna nafasi ya uzembe katika jamii.

Sentensi

Nyimbo za mawaidha zina mchanganyiko wa sentensi sahili na ambatano. Kwenye wimbo 'Warabai,' kuna sentensi fupi kama;

'Usiende, usiende mtoto wangu'.

Imedhihirika kuleta wazo la kumkataza huyu mwana asishirikiane na wageni Wamishonari. Zile ndefu zimeelezea hoja nzito katika ushauri wao kwa mfano; wakisema 'wamishonari hawajui kazi, wao hutembea tu na kulegeza mikono'.

Katika wimbo ‘Kazi anuai’ sentensi za wimbo wote ni fupi. Zimejikita katika kuelezea umuhimu wa kazi kama kulima, kuvuna, kutwanga, kusaga, usasi, na kugema.

Katika wimbo ‘nataka wa kazi’ sentensi ni ndefu ndefu katika vifungu vyote. Mwimbaji anaeleza hofu yake kwa mawazo mazito kwamba akipata mume ambaye hapendi kazi, basi atakuwa taabani. Kila mstari una maneno manne au zaidi ambacho ni kigezo cha kueleza sentensi ndefu.

Chuku

Katika wimbo ‘mtu mvivu’, mwandishi anatoa wazo la mtu kuona kazi na kuanza kuumwa na viungo vya mwili kwa njia ya chuku. Kusudi la matumizi haya ni kutilia mkazo uvivu alionao mhusika huyu na wimbo unamkosoa aache sababu ambazo hazina maana.

Ili kuonyesha kuwa Wamishonari hawafanyi kazi kama Warabai, kwenye wimbo ‘Warabai,’ wanatumia kauli ya chuku, eti kazi yao ni kutembea tu. Mtunzi wa wimbo ametilia chumvi wazo la Wamishohari kutofanya kazi wanazozifanya Warabai.

Tashihisi

Huu ni usemi wenye kukipa kitu kisicho uhai sifa ya kitu chenye uhai. Yaani ni kuvipa vitu sifa za binadamu na kuonekana kutenda kama binadamu. Wimbo ‘mtu mvivu’ una uhuishaji mara mbili. Kifungu cha pili, kiongozi wa wimbo anasema, “vidole vinakataa kazi” ikiwa na maana anayekataa kazi ni mhusika mwenyewe. Vidole havina uwezo wa kusema havitaki kufanya kazi.

Vivyo hivyo kifungu cha tatu, miguu imehuishwa na kufanywa kuwa na uwezo wa kusema kaitaki kutembea, kwenda mtoni. Hapa ni wazi kuwa mhusika mwenyewe ndiye hataki kufanya kazi hiyo ya kwenda kuchota maji mtoni.

2. 'kichwa humuuma,

vidole kukataa kazi.

3. shingo inamuuma,

miguu kukataa kwenda.

Jazanda

Jazanda ni picha anayoiona msomaji(msikilizaji) katika mawazo yake anaposoma au kusikiliza kazi yoyote ya fasihi. Neno 'tsuluni' au 'juu ya mlima', halina maana ya mlima halisi. Linaashiria mahali pazuri penye rutuba panapowezesha mimea kama migomba, mihindi au mipapayu kunawiri na kuwa na mavuno yenye faida. Hii inadhihirika katika wimbo wa 'nataka wa kazi'.

Neno 'ngoma' katika wimbo wa 'mtu mvivu' limetumiwa kama fumbo kuleta uzito wa shughuli inayotakikana kufanywa na wanajamii. Mtunzi hazungumzii 'ngoma' kama kifaa cha kutumbuiza katika sherehe bali kazi ya kushika jembe, kupanda mnazi na kuchota maji.

1. yawache, usikize ngoma ya jembe, }
rafiki, ngoma ya jembe mwenzangu } x 2

2. rafiki, ngoma ya mnazi mwenzangu, x2

3. rafiki, ngoma ya kibuyu mwenzangu, x2

Isitiari

Kamusi ya Kiswahili Sanifu(2010) inaeleza tamathali hii kuwa ni usemi unaolinganisha vitu vya aina mbili au zaidi vyenye sifa tofauti kama ilivyo katika tashbihi. Haya ni matumizi ya neno kueleza jambo ambalo maana yake ni tofauti na maana ya kawaida ya neno hilo japokuwa huwa na uhusiano wa namna fulani.

Hata hivyo tofauti na tashbihi, isitiari au sitiari haitumii maneno teule kama vile: mfano wa, kama, mithili ya au sawa na kwa mfano;

1. Ujana ni moshi,
2. Ahmed ni samba uwanjani,
3. Ambari ni fisi karamuni.

Katika kifungu cha tatu, kwenye wimbo 'nataka wa kazi', mwimbaji anamaliza kwa kumwambia shangazi yake hataki kupe ('kuhe'). Kupe kazi yake ni kumfyonza damu kutoka kwa wanyama au binadamu. Neno hili limetumika kistiari kumaanisha hangependa kamwe kuolewa na mume ambaye ataanza kumtegemea yeye katika maisha yake. Hataki mwanamume wa kumnyanyasa.

Ambaye hana kazi atanilisha nini?

Shangazi sitaki kupe.

Hitimisho:

Katika sura hii, tumebainisha jinsi ambavyo tamathali mbalimbali za semi na mbinu za kimitindo zilivyotokea katika nyimbo za kazi za jamii ya Warabai. Baadhi ya zile ambazo zimejitokeza mara kadhaa ni kama takriri, uhuishaji, misemo, jazanda na istiari. Pia matumizi ya sentensi fupi fupi kutegemea mtitimo wa kazi. Methali, chuku, balagha, kinaya zimetokea katika nyimbo hizi japo kwa kiwango kiwango kidogo sana.

Vivyo hivyo tumeweza kubainisha sifa za nyimbo za kazi kama zinavyoelezwa na Kinoti (2008). Katika kuelezea sifa hizo anasema kuna:

Matumizi ya maneno mepesi yaliyo rahisi yakuweza kujifunza na kuimba papo hapo. Kwa mfano wimbo wa 'kulima', kutwanga' na 'kusaga'.

Takriri-maneno na sauti zinazorudiwarudiwa ili kuoana vilivyo nan a matumizi ya tanakali za sauti, kwa mfano, jinsi mchi unavyodunda kwenye kinu. Kwa hivyo urudiaji pia unategemea kazi inavyofanywa.

Kupokezana-kiongozi wa wimbo hupokezana na wenzake. Karibu nyimbo zote za kazi zimedhihirisha sifa hii ya kupokezana.

Maneno, sauti na milio isiyo na maana maalum mradi iweze kujenga mdundo wa nyimbo, kwa mfano, wimbo wa 'mchungaji wangu'-'mrisa wangu ga'. Hicho kijishemu cha 'ga' hakina maana fulani bali ni mbinu ya kuondoa uchovu wakati wa kazi.

Madoido na vigelegele ili kuufanya wimbo kuvutia, kwa mfano, wimbo wa 'Warabai'.

Maneno ya nyimbo zenyewe ni za kuhimiza. Kwa mfano, wimbo wa 'kazi ni leo'.

Mdundo nao hutegemea kazi inavyofanywa. Iwapo kazi itafanywa kwa kasi, mdundo utakuwa wa kasi. Kazi ikiwa inafanywa taratibu, mdundo nao unafuata hali hiyo.

SURA YA NNE

4.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumeshughulikia muhtasari wa tasnifu kutoka sura ya kwanza hadi ya nne kuhusu mbinu za kimtindo katika nyimbo za kazi za jamii ya Waraba.

Mbinu za utafiti zilizotumika ni za nyanjani ambapo tulipata data (nyimbo) tulizochanganua. Vivyo hivyo utafiti wa maktabani ulisaidia.

Tumeeleza matokeo ya utafiti, mafanikio pamoja na changamoto tulizokumbana nazo. Hali kadhalika, tumetoa mapendekezo ya tafiti zingine ambazo zinaweza kufanywa kuhusu uwanja huu tulioshughulikia.

4.1 Muhtasari wa utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchanganua mbinu za kimtindo katika nyimbo za kazi za jamii ya warabai. Katika kufanya hivyo nadharia ya kimtindo ilitumika katika kazi hii. Tulishughulikia nyimbo kumi na tano za Kirabai. Nyimbo zenyewe tulizishughulikia katika viwango vifuatavyo;

- a) Tamathali za semi
- b) Mbinu za kimtindo
- c) Miundo ya sentensi na msamiati

Sura ya kwanza katika tasnifu hii, imezungumzia mada tuliyoifanyia utafiti. Katika kushughulikia swala hili, tumejadili swala la utafiti na kuonyesha kusudi letu la kufanya

utafiti huu. Vivyo hivyo, tumelezea nadharia ya kimtindo ilivyotumika na kilichotufanya kuteua sawala letu na upeo wa kazi wenyewe.

Sura ya pili tumejadili jamii ya Warabai yaani makazi yao. Pia tumeangalia utamaduni wa jamii hii. Umuhimu wa kuangalia mambo haya ni kutoa mwangaza kwa kazi iliyokuwa inatafitiwa hasa kwa kueleza zaidi shughuli zao zinazohusiana na kazi mbalimbali.

Katika sura ya tatu, tumejadili nyimbo kumi na tano zilizoimbwa wakati wa shughuli tofauti za kazi katika jamii ya Warabai. Nyimbo zenyewe zimetafsiriwa kwa Kiswahili na uchanganuzi wa matumizi ya lugha na mbinu za kimtindo ukafanywa.

Katika kufanya hivyo makundi mbalimbali yaliziimba nyimbo hizo walipokuwa wakifanya kazi hizo. Pia mtafiti aliweza kuchukua picha kadhaa pale ilipowezekana.

4.2 Matokeo ya utafiti

Shabaha kubwa ya somo la fasihi simulizi ni kumsaidia mja kuwasiliana kwa njia ya kumpendeza na kujitumbuiza hasa kupitia matumizi ya lugha yenye kunasa akili na kuisimua hisia. Kwa kutimiza hayo fasihi simulizi imekuwa na itabakia hai yenye kumfunza na kumwongoa insi katika maisha yake.

Katika kazi hii, imebainika wazi kuwa, nadharia ya kimtindo ndiyo iliyokuwa mwafaka kabisa, kwani aliyoyasema Ngara (1981) kuhusu lugha yamebainika katika nyimbo za kazi za jamii ya Warabai.

Haja yetu ya utafiti ilikuwa kuchunguza kama inawezekana vipengele vinavyounda lugha (tamathali za semi) na mbinu za kimtindo kutumika katika nyimbo za kazi. Imedhihirika kwamba matumizi ya lugha na mbinu za kisanaa katika nyimbo za kazi, kwa asilimia kubwa ni lugha bayana au ile inayoitwa lugha kavu (Msokile; 1983).

Maoni hayo ya Msokile yameafikiana kabisa na utafiti wetu kwani tamathali za semi zilizojitokeza zilikuwa ni zile zile yaani takriri, nidaa, tashbihi, istiara na jazanda. Kati ya hizi, takriri au urudiaji umejitokeza katika nyimbo zote za kazi tulizozichanganua.

Hii ni kwa sababu kazi zinapofanywa huwa na ile hali ya kuitelekeza kwa njia ya kurudiarudia. Matumizi mengine ya takriri yalilenga kusisitiza kile mtunzi alichotaka katika kazi yenyewe. Kwa mfano, kama anasisitiza kazi ya kutwanga au kusaga, basi maneno hayo yamerudiwarudiwa katika nyimbo hizo.

Nyimbo nyingi zilikuwa na sentensi fupi fupi na nyingine zikawa na mchanganyiko wa sentensi sahili na changamano. Sentensi hizi ziliashiria midundo ya kazi ilivyokuwa ikiendelea.

Sentensi fupi zilidhihirisha midundo ya haraka haraka, nazo ndefu wakati mwingine, ziliweza kuonyesha utaratibu wa kazi fulani.

Tamathali ya semi kama methali, haikujitokeza sana katika nyimbo hizi za kazi. Mbinu za kimtindo kama taswira, chuku na kinaya pia hazikujitokeza sana.

Tumeweza kutambua kuwa asilimia kubwa ya nyimbo za kazi ziliimbwa na wanawake ikilinganishwa na zile zilizoimbwa na wanaume. Jambo hili lilithibitishwa na Jones (1987)

anaposema;

“Utamaduni hasa wa kiafrika unamdunisha mwanamke kwa kumpa majukumu (kazi) mengi katika jamii hali mwanamume ndio mtawala wa jamii.”

(Tafsiri yetu)

Kadhalika tumebainisha kuwa siku hizi nyimbo hizi haziimbwi sana kutokana na mabadiliko ya maisha. Kupitia mahojiano yasiyoratibiwa tumeweza kuelewa kuwa baadhi ya kazi kama kutwanga, kupepetana na kusaga hazifanywi sana na wanajamii kama zamani kwani kuna mitambo inayofanya kazi hizo mara moja. Mambo haya yanathibitishwa na Shitemi (2006), anaposema;

“Fasihi simulizi kama ilivyo fasihi kwa jumla imeathiriwa na mabadiliko na uchangamano wa tamaduni zetu.”

Anaendelea kueleza kuwa mipaka ya mila na utamaduni inazidi kupomoka na kuchangamana kiasi kuwa fasihi simulizi inayoinuka, hasa katika maeneo ya kimji, haiakisi utamaduni maalumu tunavyofahamu kijadi.

Tumeweza kwa kiasi kikubwa kufanikiwa na kutambua kuwa nyimbo za kazi za jamii ya warabai zinaweza kuwa na lugha na mtindo wa kipekee kama ilivyo katika tanzu zingine za fasihi simulizi.

Hali kadhalika tumefanikiwa kuonyesha kwamba nyimbo hizi pia zinaweza kutumiwa kama tanzu zingine za kifasihi kufunzia lugha.

Jamii yapaswa kutilia maanani nyimbo hizi za kazi hasa kufunza kizazi chipukizi ili tusipoteze sehemu muhimu ya utamaduni wa Mwafrika.

4.3 Mapendekezo kwa utafiti ufuatao

Utafiti wetu umejhusisha na matumizi ya lugha na mbinu za kimtindo katika nyimbo za kazi ya jamii ya Warabai.

Tumepata ufanisi kuona matumizi ya lugha na mbinu kadhaa za kimtindo zimedhihirika katika nyimbo hizo. Hata hivyo, kuna mengi ambayo hatukushughulikia na ambayo mtafiti mwingine yeyote angeweza kuyachunguza:

Utafiti ufanywe kuhusu matumizi ya lugha na mbinu za kimtindo za nyimbo za kazi katika lugha zingine kama vile Kikikuyu, Kiluhya, Kidholuo na Kikamba. Hii ni kwa sababu utafiti wetu ulishughulikia nyimbo za jamii ya Warabai (Mijikenda) pekee.

Umuhimu wa utafiti kama huu utaweza kubainisha kama nyimbo zina ulinganifu na sifa sawa. Mtafiti pia aweze kutoa sababu za tofauti hizi.

Tunapendekeza utafiti ufanywe kuhusu mabadiliko yoyote yaliyoko katika nyimbo za kazi za jamii ya Warabai na jamii nyingine za Kiafrika. Hii ni kwa sababu utafiti wetu,

uliangalia nyimbo hizo kwa ujumla bila kushughulikia vipindi mbalimbali. Utafiti kama huu utasaidia kwani kuna mabadilijiko mengi ya kiteknolojia na huenda yameathiri nyimbo hizi za kazi. Ni matumaini yetu kuwa utafiti wa aina hii ukifanywa mila na tamaduni za kiafrika zitaeleweka na kupewa hadhi inayofaa. Hali kadhalika utafiti unaweza kufanywa kwa kuchunguza umuhimu wa maudhui yanayowasilishwa na nyimbo za kazi kwa kizazi cha sasa.

Tunapendekeza utafiti ufanywe juu ya maudhui ya kiuana, hasa mtazamo wa kundi la Mijikenda kuhusu mwanamke. Hii ni kwa sababu nyimbo nyingi tulizozipata zinahusu kazi ambazo zinafanywa na wanawake kama vile kulima, kutwanga, kupepete na kusaga. Mwisho tunapendekeza utafiti ufanywe kuhusu nyimbo zingine kama za harusi, matanga, nyiso na bembelezi katika jamii hii ya Warabai.

4.4 Changamoto za utafiti huu

Utafiti ulikuwa wa kupendeza na wa kufana kwani tulitimiza malengo yetu. Hata hivyo tulikumbana na changamoto kadha wa kadha:

Ukosefu wa hela za kutosha. Usafiri ulikuwa ghali sababu ya safari za kwenda pwani ili kupata data. Data ilikusanywa kati ya mwezi wa tatu na wa saba. Ilibidi safari ziwe nyingi ili kukutana na makundi mbalimbali. Fedha pia zilihitajika kununua kaseti zilizotumika sana. Pia wasaidizi walihitaji fedha kusafiria kwa maeneo hayo matano tuliyoyachagua.

Baadhi ya shughuli za kazi hazikuwa na watendaji kazi kama uvunaji wa asali kwa hivyo ikawa vigumu kupata nyimbo za kazi hiyo. Sababu kubwa tuliambiwa wenyeji wameingilia zaidi kazi ya ugemaji na kutotilia mkazo kazi hii ya uvunaji wa asali.

Makundi machache hayakushirikiana kwa ukamilifu na wasaidizi wetu. Hasa wanaume hawakupatikana kwa kazi kama za kulima. Hawakupenda hata mambo ya picha kwa sababu ambazo huenda ni za kitamaduni. Wanawake walishirikiana vyema na mtafiti pamoja na wasaidizi wake.

Tulipata pia matatizo ya kutafsiri baadhi ya nyimbo hizo. Baadhi ya vifaa walivyovitumia kwa kazi kama ya kusaga, hutumia 'lwala', hatukupata neno moja la kueleza ila tulitafsiri tu kuwa ni 'jiwe la kusaga'. Maneno mengine yalipotafsiriwa yaliweza kupoteza maana asili.

Katika shughuli kama ya kutwanga, ilibidi mtafiti kuwaomba wanaofanya kazi hiyo waimbe. Hili pia halikiwa jambo rahisi kwa baadhi ya maeneo.

Hitimisho

Ingawa bado kuna jamii kama Wamasaai na Wakalenjin wanaoimba wakati wa kazi, mambo yamebadilika pakubwa. Ni vigumu wanaofanya kazi ofisini kuziimba nyimbo jinsi zilivyoimbwa katika siku za jadi kwa mfano, kazi nyingi ofisini zinahitaji kufanywa kwa utulivu usioruhusu kelele.

Japo hivyo, maendeleo ya kiteknolojia mengi yametokea. Kwa wakati huu kuna redio na CD zinazowekwa kwenye tarakilishi, ambazo huimba watu wanapofanya kazi. Kwa hivyo mfanyikazi hujiunga na waimbaji katika redio au akachangamka tu na kujipa shime kisikiliza huku akiendelea kufanya kazi.

MAREJELEO

Abudu, M. (1974): *Methali za Kiswahili, Maana na Matumizi*. Nairobi.

Foundations Books.

Adagala, K. na Wengine. (1995): *Kenyan Oral Narratives*. Nairobi. East African

Educational Publishes.

Ahmed, S. (1978): *Lugha, Tungo na Msamiati wa Kiswahili*. MULIKA NA 14. Dar

es Salaam.

Bakari, E. (1988): *Kilifi District Socio-Cultural Profile*. (Project Director Draft).

Institute African Studies. University of Nairobi.

Balisidya, M. (1987) "*Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi*" Mulika 19. Dar es Salaam.

TUKI.

Bauman, R. (1977). *Verbal Art as Performance*. Rowley: Newbury House

Chesaina, C. (1991). *Oral Literature of the Kalenjin*. Nairobi. Heinemann Kenya

Coombes, H. (1953). *Literature and Criticism*. London. Penguin Books

Finnegan, R. (1970): *Oral Literature in Africa*. East Africa. Oxford University Press

Halliday, M (1978). *Language as a Special Semeotic. The Social Interpretation of*

Language and Meaning. London

Ifedha, A. (1987): *Semi za Kiswahili*. Nairobi. Oxford University Press

Jones, E na wengineo (1987). *Women in African Literature Today*. London: African
World Press.

Justin, W. (1980): "*The Mijikenda and Mombasa to 1930*" (Thesis for Phd Degree.
School Oriental and African Studies. University of London).

Kabira, W. (1983): *The Oral Artist*. Nairobi. East African Foundational Publishers.

Kabira, W. na Kaega, M (1988): *Gikuyu Oral Literature*. Nairobi. Heinemann Kenya
Ltd.

Kagwa, F. na Gichohi, W. (2011): *Kamusi Fafanuzi ya Misemo*. Nairobi:
Target Publications Limited.

Kamusi Kamili ya Kiswahili (2009): Nairobi. Longhorn –publishers.

Kapiyo na Wengine (2003): *The Evolving World. History and Government Course*.
Oxford University Press.

Kenya Institute of Education (2004): *Kiswahili Kitukuzwe: Kidato cha Kwanza*.
Nairobi. Kenya Literature Bureau.

Kilauni, N (2007): "*Usasa Katika Nyimbo za Itheke*" (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu
Cha Kenyatta).

- Kinoti, T. (2008): *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi. The Jomo Kenyatta Foundation.
- King'ei, G. (1992): "*Language, Culture and Communication. The Role of Swahili, Taarab Songs in Kenya from 1963-1990*". (Unpublished Phd. Dissertation, Harvard University. America)
- King'ei, G. na Kisovi, C. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi. Kenya Literature Bureau.
- Kipury, N. (1983): *Oral Literature of the Maasai*. Nairobi. Heinemann Kenya
- Kombo, D. na Wengine (2006): *Proposal and Thesis Writing*. Nairobi. Pauline's Publications Africa.
- Kothari, C (2004). *Quantitative Techniques 2nd Edition*. New Delhi. India: New Age International Ltd.
- Kuhenga, C. (1986): "*Tamathali za Semi za Kiswahili*" MULIKA NA 13. Dar es Saalam. TUKI.
- Leech, G. and Short, M. (1981): *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Functional Prose*. New York. Longman Group Ltd.

Leech, G. (1969): *A Linguistic Guide to English Poetry*. London. Longman Group Ltd.

Lindfords, B. (1991): *Popular Literature in Africa*. Triton New Jersey. India

University Press.

Malenya, M. (2008): "*Matumizi ya Lugha na Jazanda Katika Nyimbo za Jacob*

Luseno" (tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta).

Masinde, E. (1992): "*Mashairi-Huru: Uchambuzi Wa Dhamira na Mtindo*". (Tasnifu

Ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta).

Mbogo, S. (2008): "*Mabadiliko ya Maudhui Kiwakati Katika Nyimbo za Harusi za*

Jamii ya Waembu". (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta).

Milroy, L. (1987): *Observing and Analyzing Natural Languages*. Oxford Basil

Blackwell Ltd.

Miruka, O (1994): *Encounters with Oral Literature*. Nairobi. East African

Educational Publishers.

Mohamed, S. A. (1995): *Kunga za Nathari za Kiswahili*. Nairobi, E.A.P.H.

Mohamed, S. K. (1986): "*Tamathali za Semi za Kiswahili*": MULIKA NA 18: Dar es

Salaam. TUKI.

Msokile, M. (1993): *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. East African Educational Publishers.

Mugenda, O. na Mugenda, A. (2003): *Research Methods. Quantitative Approaches*. Nairobi Acts Press.

Mulokozi, M. (1989): "*Tanzu za Fasihi Simulizi*" MULIKA NA 21: Dar es Salaam, TUKI.

Mutai, B. (2000). *How to Write Quality Research Proposal*. Thelley Publications.

Mutwiri, G. (2005): "*Mitazamo ya Utendakazi wa Nyiso Katika Jamii ya Watigania*" (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta).

Mwai, K. (1997): "*The Power of Song for Swahili Woman. Contesting Social Death*". *Essay on Gender and Culture*. Nairobi. K.O.L.A.

Mwangudza, J (1983): *Kenya's People: Mijikenda*. Nairobi. Evans Brothers.

Mwaniki, M. (2011): "*Matumizi ya Lugha Katika Nyimbo Tohozi za Salim Junior*" (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta).

Mwanzia, P. (2007): "*Mtindo wa Nyimbo za Watoto wa Shule za Chekechea*" (Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Kenyatta).

Nandwa, J. na Bukenya, A. (1983): *African Oral Literature for Schools*.

Nairobi. Heinemann.

Nathan, O. na Wengine wahariri (2008): *Nadharia Katika Taaluma ya Kiswahili na*

Lugha za Kiafrika. Eldoret. Moi University Press.

Ngara, E. (1981): *Stylistic Criticism and the African Novel*. Ibadan. Heinemann.

Ngowa, N. (2007): *"Mnyambuliko wa Vitenzi vya Kigiriyama: Mtazamo wa*

Fonolojia Leksishi" (Tanifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta).

Ngugi, T (1986): *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African*

Literature. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Ngure, A. (2003): *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari*. Nairobi. Print Limited.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999): *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*.

Nairobi Jomo Kenyatta Foundations.

Njogu, K. na Wengine (2006): *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Nairobi.

Twaweza Communications.

Nkonge, K (1988): *"Literary Study of Songs of Joseph Kamaru, Theme and Style"*

(Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta).

Ntarangwi, M. (1990): *“Uhakiki wa Maudhui ya Utetezi Katika Utunzi wa*

Ramadhani Ongara” (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta).

P’ Bitek, O. (1973): *African Cultural Revolution*. Nairobi. Macmillan.

Ruo, K. R. (1989): *Nguzo za Ushairi wa Kiswahili*. Nairobi. Macmillan Kenya.

Senkoro, F. (1978). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam. Press and Publishing Centre.

Shitemi, N. (1978): *Fasihi Simulizi Katika Miktadha ya Matumizi ya Lugha, Kisanii*

na Kiamali. (Makala za Semina ya Kimataifa).

Spear, T (1948): *The Kaya Complex: A History of the Mijikenda People of the*

Kenyan Coast to 1900. Nairobi. Kenya Literature Bureau.

Spolky, B (1988): *Sociolinguistics*. Oxford. Oxford University Press.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. (1981): *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi.

Oxford University Press.

Traugott, E. and Pratt, M. (1980): *Linguistics for Students of Literature*. New

York. Harcourt.

Turner, G (1973): *Stylistics*. New York. Hazel. Watson and Viney Ltd.

Wafula, R. na Njogu, K. (2007): *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. Jomo

Kenyatta Foundation.

Waihiga G. Na Wamitila, K. (2005): *Chemichemi za Kiswahili: Kidato Cha Pili*.

Nairobi Longhorn Publishers.

Waititu na Ipara, O. (2008): *Kiswahili Fasihi Kidato Cha Nne*. Nairobi. Oxford

University Press.

Wambua, S. (2001): "*Mtindo wa Nyimbo za Kakai Kilonzo*" (Tasnifu ya Uzamili,

Chuo Kikuu Cha Kenyatta).

Wamitila, K (2008): *Kichecheo Cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi. Focus Publications.

_____ (2003): *Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia*. Nairobi. Focus Publications

_____ (2004): *Chemichemi za Kiswahili. Kidato Cha Tatu*. Nairobi.

Longhorn Publishers.

Wanjala, S. (2001): "*Nyiso za Wabukusu: Maudhui na Lugha*" (Tasnifu ya Uzamili,

Chuo Kikuu Cha Kenyatta).

Wanyama, A. (2006): "*Maudhui na Mtindo Katika Utendi wa Wabukusu:*


Khuswala Kumuse" (Tasnifu Ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta).

Wellek R. na Warren, A. (1970): *Theory of Literature*. New York. Harcourt.

Yalwala, P (1991): "*Maudhui Katika Nyimbo za John Mwale*" (Tasnifu za Uzamili,

Chuo Kikuu Cha Nairobi).

KIAMBATISHO 1: RAMANI



Ramani ya makaazi ya Warabai na jamii zingine za Kimijikenda.

KIAMBATISHO 2

Habari kuhusu utamaduni wa Warabai, tulizipata kupitia mahojiano yasiyo ya muundo kutoka kwa wahusika wafuatao: -

- 1) Babu Ndaro
- 2) Babu Chengo
- 3) Bibi Mkambe
- 4) Bibi Wedzuware

Ilikuwa tarehe 27 Aprili 2011

KIAMBATISHO 3: NYIMBO ZA KIRABAI ZILIZOCHANGANULIWA

Wimbo wa kwanza

Kurima, kuhonda na kusaga

1. Jembe, ee jembe dodomera x2 – Kiongozi

Atu achirima

Arimadze? } X2

nami nikarime vivyo vivyo wote

2. Chinu, ee chinu dodomera x2 - Kiongozi

atu achihonda

Ahondadze? } x2

nami nikahonde vivyo vivyo wote

3. Lwala, ee lwala dodomera - X2 – kiongozi

atu achisaga

Asagadze? } x2

nami nikasage vivyo vivyo ? wote

Tafsiri

1. Jembe , ee jembe makinika

watu wakilima

} x2 kiongozi

wanalima vipi?

nami nikalime vivyo hivyo } x2 wote

2. Kinu, ee kinu makinika

watu wakitwanga } x2 kiongozi

wanatwanga vipi?

nami nikatwange vivyo hivyo } x2 wote

3. Jiwe la kusaga ee, makinika

watu wakisaga } x2 kiongozi

wanasaga vipi?

nami nikasage vivyo hivyo } x2 wote

Wimbo wa pili

Nahonda

Nahonda, nahonda,

kisha nisage,

ga baba sindagaweza,

} Kiongozi

mayo yunadza machero,

machero dzua ra haho.

Nahonda, nahonda,

kisha nisage,

ga baba sindagaweza,

mayo yunadza machero,

machero dzua ra haho.

Tafsiri

Natwanga, natwanga

kasha nisage

ya baba sitayaweza

mama atakuja kesho

kesho machweo

} kiongozi

Natwanga, natwanga

kasha nisage

ya baba sitayaweza

mama atakuja kesho

kesho machweo

} x2 wahusika wawili au watatu

Wimbo wa tatu

Kuhonda na kusaga

Atu ni kuhonda, akasaga x2

sagani, sagani mudze hurye,

} kiongozi

mengolowe hee! hee! x2

atu ni kuhonda, akasaga x2

sagani, sagani mudze hurye

} wote

mengolowe hee! Hee! X2

Tafsiri

Watu hutwanga, wakasaga x2

sageni, sageni mje tule

mamake ngolo, hee! hee! x2

} x2 kiongozi

watu hutwanga, wakasaga x2

sageni, sageni mje tule

mamake ngolo, hee! hee! x2

} x2 kiongozi

Wimbo wa nne

Kusaga

1. Namjeni wangu ee,

kalala na nzala,

meye Mwaka, uwe

} kiongozi

saga unipe lwala

Namjeni wangu ee,
kalala na nzala,
meye Mwaka, uwe,
saga unipe lwala

} wote

2. Namtsedza wangu ee,
kalala na nzala,
meye mwaka, uwe,
saga unipe unga.

} kiongozi

Namtsedza wangu ee,
Kalala na nzala,
Meye mwaka, uwe,
Saga unipe unga.

} wote

3. Nina mwanangu ee,
kalala na nzala,
meye Mwaka, uwe,
saga unipe wari

} Kiongozi

Nina mwanangu ee,
kalala na nzala,
meye Mwaka, uwe,
saga unipe wari

} wote

Tafsiri

1. Nina mgeni wangu ee,
halali na njaa
mamake mwaka wee,
saga unipe hilo jiwe

} kiongozi

nina mgeni wangu ee,
halali na njaa
mamake mwaka wee,
saga unipe hilo jiwe

} wote

2. Nina mke wangu ee,
halali na njaa
mamake mwaka ee,
saga unipe unga

} kiongozi

nina mke wangu ee,
halali na njaa
mamake mwaka ee,

} wote

saga unipe unga

3. Nina mtoto wangu ee,
halali na njaa
mamake mwaka ee,
saga unipe ugali
- } kiongozi
- nina mtoto wangu ee,
halali na njaa
mamake mwaka ee,
saga unipe ugali
- } wote

Wimbo wa tano

Kuheheta:

Kadzo heheta, heheta, muhama x2 } Kiitikio

Kadzo heheta, heheta – Wote

1. Kadzo yundanwa,
muswa wa muhama.
- } kiongozi

Kadzo heheta, heheta,
ni wari hundarya.

} wote

2. Kadzo manya lutsanga,
ludzale muhama
- } kiongozi

Kadzo heheta, heheta } wote
na nzala isidzone. }

Tafsiri

Kadzo pepeta, pepeta mtama x2 }
Kadzo pepeta, pepeta-wote } kiongozi

1. Kadzo atakunywa } kiongozi
uji wa mtama }
kadzo pepeta, pepeta }
na ugali tutakula } wote
2. Kadzo hakikisha ghala }
ziweze kujaa mtama } kiongozi
kadzo pepeta, pepeta }
na njaa isijione } wote

Wimbo wa sita

Mrisa wangu

Mrisa wangu ee, }
mrisa wangu ga, }
mrisa wangu wee, } kiongozi

kanwa maziya.

Mrisa wangu ee,
mrisa wangu ga,
mrisa wangu wee,
kanwa maziya. } wote

ndamwambira baba – kiongozi

mrisa wangu ee,
kanwa maziya. } wote

maziya ganaguzwa – Kiongozi

mrisa wangu ee,
kanwa maziya } wote

kaziye dza nzovu – kiongozi

mrisa wangu ee,
kanwa maziya } wote

achirya dza tsungu - kiongozi

mrisa wangu ee, } wote

Kanwa maziya.

Tafsiri

Mchungaji wangu ee,
mchungaji wangu aa,
mchungaji wangu wee,
hanywi maziwa

} kiongozi

mchungaji wangu ee,
mchungaji wangu aa,
mchungaji wangu wee,
hanywi maziwa

} x2 wote

nitamwambia baba – kiongozi

mchungaji wangu wee,
hanywi maziwa

} x2 wote

kazi yake ni kama ya ndovu - kiongozi

mchungaji wangu wee,
hanywi maziwa

} x2 wote

akila ni kama chungu - kiongozi

mchungaji wangu wee,
hanywi maziwa } x2 wote

Wimbo wa saba

Kurisa

1. Kurisa ni kuhala mifugo,
kwenda nao vueni,
kwenda uimirire, urise,
dza mbuzi, ng'onzi na ng'ombe.
Nahurise, nahurise x2 – Kiongozi } kiitikio
Anadza ahokole x2 – wote }
2. Unaamboza madzacha, ichifika dziloni
unaaudzya aoye,
unaaudzya nyumbani, mpaka machero
ao mbuzi, kondoo na ngo'mbe

Tafsiri

1. Kuchunga ni kuchukua mifugo

kwenda nao msituni (malishoni)

kwenda nao uwasimamie, uwalishe

kama vile mbuzi, kondoo na ngombe

natuchunge, natuchunge x2 kiongozi

watakuja kutuokoa x2 wote

}
} kiitikio

2. Unawatoa asubuhi, ukifika jioni

unawarudisha wapumzike

unawarudisha nyumbani wapumzike hadi kesho

hao mbuzi, kondoo na ngo'mbe

Wimbo wa nane

Nikamdunge ng'ombe wangu

1. Nifugurira miryango,

na senzi ulongo,

daktari nahenza sindano,

nikamdunge ng'ombe wangu x2

2. Na unipe mawaidha,

nahenza anifaidi,

daktari nahenza sindano,

nikamdunge ng'ombe wangu x2

3. Mbiri zamshinda fisi,
mfugadzi nikwenda na mosi,

daktari nahenza sindano,

nikamdunge ng'ombe wangu. x2

Tafsiri

1. Nifungulie mlango

na sitaki uongo,

daktari nataka sindano,

nikamdunge ngombe wangu x2

2. Nipatie mwaidha

nataka unifaidi

daktari nataka sindano

ni kamdunge ngombe wangu x2

3. Mbili zilimshinda fisi,

mfugaji huenda na moja,

daktari nataka, sindano

nikamdunge ngombe wangu x2

Wimbo wa tisa

Kujema

Kujema kuna faidaa, }
kazi ya kujema aa, }
ni kunola luhamba, } kiongozi
uhale ndere ukwere, }
dzulu ya mnazi. }

Mnazi una faidaa, }
Una kazi mbidzo, } wote

Una mutswanowe, }
dza asali ya nyuchi, } x2 wote

Abgwiraye handaa, }
aritsinze na luhamba, } kiongozi
avugule atsinze ouchi umbole, }
Achiguza yu tototo we, }

Tafsiri

Kugema kuna faidaa,
kazi ya kugema aa,
nikikinoa kile kisu,
uchukue kibuyu upande
juu ya mnazi

} kiongozi

mnazi una faidaa x2 –kiongozi

una kazi nzuri,
una utamu wake,
kama asali ya nyuki

} wote

alishike tagaa,
alicate kwa kisu,
afungue akate, tembo litoke
akiuza yuko sawa wee

} kiongozi

Wimbo wa kumi

Ujemaji

Mbunge wehu Chibule,

hunahenza kumanya,

kurayo, 'iriyo indakudza,

hunamala uuye bunge dede,

kiongozi

hupate kumanya naswi, hunanya ng'anywa.

Mjema; mjema yunarira,

ajemerwaye naye yunarira,

hindeni kwa Chibule,

ndiye yundahokola.

x2

wote

Tafsiri

1. Mbunge wetu Chibule,
tunataka kujua,
uchaguzi ambao unakuja,
tunataka urudi bunge mwenzetu,
uweze kujua sisi tunanyang'anywa

kiongozi

mgema, mgema analia,
anayegemewa pia analia,
twendeni kwa chebule,
ndiye atatuokoa

} x2 wote

Wimbo wa kumi na moja

Kujenga

1. Mtu achihenza kujenga, x2 – Kiongozi

Nikuhumira mihi hebu mawe,
kutsimba mashimo msingiwe,
ndo aweze kwenda dzulu.

} wote

Yo nyumba 'idza 'iva? - Kiongozi

2. Mtu achihenza kujenga x2 – kiongozi

mahalu nikukala gana vimbwa
makuti nago ganavimbwa,
kazi ya nyumba idzagoma.

} wote

Yo nyumba idza 'iva? – Kiongozi

3. Mtu achihenza kujenga x2 – Kiongozi

yunahumira fiho na papi,
misumari kukokota mabati,
seze kuinjira na kulala,

} wote

Yo nyumba idza iva? – kiongozi

Tafsiri

1. Mtu anataka kujenga x2 kiongozi

hutumia miti au mawe
huchimba mashimo ya misingi,
ndio aweze kupandisha juu
hiyo nyumba imeiva? - kiongozi

} wote

2. Mtu akitaka kujenga x2-kiongozi

paa huwa linaezekwa,
makuti pia huezeka,
kazi ya nyumba imeisha

} wote

hiyo nyumba imeiva?- kiongozi

3. Mtu akitaka kujenga – x2 kiongozi

hutumia fito au pau,
misumari kugongelea mabati,

} wote

bado kuingia na kulala

hiyo nyumba imeiva?- kiongozi

Wimbo wa kumi na mbili

Arahai

Ano baba, ano mayo, Arahai,

ni kunena makaamba,

amisheni kaajema, kaarima,

kazi yao ni kutsembera,

na mikono lewe lewe

} kiongozi

Usende, usende mwanangu,

usende undapambazwa.

} x2

} wote

Pekeshe mwambire mulamu yunadza,

pekeshe dzua rinagoma aah,

yunarira – kiongozi

howaa, mwanangu, howaa – wote

Tafsiri

Akina baba, akina mama, Warabai

huzungumza na kusema,

wamisheni hawagemi, hawalimi

kazi yao ni kutembea,

na mikono lege lege

x2 kiongozi

usiende, usiende mwanangu

usiende utapumbazwa

x2 wote

pekeshe mwambie mjomba anakuja,

pekeshe jua linaisha aah,

yualia - kiongozi

howa, mwanangu howaa x2 wote

Wimbo wa kumi na tatu

Mtu mkaha

1. Mtu mkaha, achona kurima,

lubavu lunamuluma,

luhosi lunampiga,

maneno manji ga kuririra wari

kiongozi

Gariche, usirikize ngoma ya jembe dede }x2
Asena, ngoma ya jembe dede } wote

2. Mtu mkaha achona kujema, }
chitswa chinamuluma, } kiongozi
vyala kavyenzi kazi, }
maneno manji ga kuririra wari, }

gariche, usirikize ga kukwera mnazi, }
asena, ngoma ya mnazi dede. } wote

3. Mtu mkaha achambwa muhoni, }
tsingo inamuluma, } kiongozi
magulu kagenzi kwenda, }
maneno manji ga kuririra wari }

gariche, usirikize ga tirinje, }
asena, ngoma ya tirinje dede } wote

Tafsiri

1. Mtu mvivu akiona kulima,
mbavu humuuma,
utosi unamdunda,
maneno mengi ya kulialia ugali } kiongozi

yawache, usikize ngoma ya jembe,
rafiki, ngoma ya jembe mwenzangu } x2 wote

2. Mtu mvivu akiona kugema,
kichwa humuuma
vidole kukataa kazi
maneno mengi ya kulialia ugali } kiongozi

yawache, usikize ya kukwea mnazi,
rafiki, ngoma ya mnazi mwenzangu } x2 wote

3. Mtu mvivu ukimwambia mtoni
shingo inamuuma
miguu kukataa mwenda,
maneno mengi ya kulialia ugali } kiongozi

yawache, usikize ya kibuyu, }
}

rafiki, ngoma ya kibuyu mwenzangu x2 wote

Wimbo wa kumi na nne

Namala wa kazi

1. Naunyala tsuluni wo mgomba, mdunda tsi,
namala wa kazi tsangazimi x2

asiyekazi andanipa noni?

tsangazimi namala wa kazi.
2. Naganyala tsuluni go matsere,
namala wa kazi tsangazimi x2

asiyekazi yundanivisha noni?

tsangazimi namala wa kazi.
3. Nainyala tsuluni yo mipapayu,
namala wa kazi tsangazimi x2

asiyekazi yundanirisani mino?

tsangazimi senzi kuhe dede.

Tafsiri

1. Naupanda juu ya mlima huo mgomba,

nataka mwenye kazi shangazi x2

ambaye hana kazi atanipa nini?

shangazi nataka mwenye kazi

2. Nayapanda juu ya mlima hayo mahindi,

nataka mwenye kazi shangazi x2

ambaye hana kazi atanivisha nini?

shangazi nataka mwenye kazi

3. Naipanda juu ya mlima mipapayu

nataka mwenye kazi shangazi x2

ambaye hana kazi atanivisha nini?

shangazi sitaki kupe

Wimbo wa kumi na tano

Makazi

1. Haya wee! x2 makazi ni rero
kuna makazi ga kurima } kiongozi

makazi ni rero – wote

kuna makazi ga kuvuna – kiongozi

makazi ni rero } x2

naavoya wee! } Wote

2. Haya wee! x2 makazi ni rero, } Kiongozi
kuna makazi ga kuhonda. }

makazi ni rero – wote

kuna makazi ga kusaga – kiongozi

makazi ni rero, }
naasihi wee! } x2 wote

3. Haya wee! x2 Makazi ni rero, } Kiongozi
kuna makazi ga kuinza, }

makazi ni rero – wote

kuna makazi ga kujema - kiongozi

makazi ni rero } Wote
mugamanye dede! }

Tafsiri

1. Haya wee! x 2 kazi ni leo }
kuna kazi ya kulima } kiongozi

kazi ni leo – wote

kuna kazi ya kuvuna – kiongozi

kazi ni leo,
nawaomba wee! } x2 wote

2. Haya wee! x 2 kazi ni leo }
kuna kazi ya kutwanga } kiongozi

kazi ni leo – wote

kuna kazi ya kusaga – kiongozi

nawasihi wee! x2 kazi ni leo-wote

3. Haya wee! x 2 kazi ni leo }
kuna kazi ya kusasi } kiongozi

kazi ni leo – wote

kuna kazi ya kugema – kiongozi

kazi ni leo
myajue wenzangu wee! } x2 wote

KIAMBATISHO 4



MTAFITI ASHIRIKI KATIKA KAZI ZA KUTWANGA



AKINA MAMA WAKIPEPETA



AKINA MAMA WAKISHIRIKI KULIMA KWA MENYAMVULA



MTAFITI AKISAGA



KIJANA JACKA AKIPANDA MNAZI

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY